

MSIKIENI YEYE



“... imani itawaokoa wagonjwa, naye Mungu atawainua.”
[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mwaweza kuja huku, ndugu, tuweze kuwawekea hawa mikono yetu? Najua katika hili, daima tumewasikia wakiuliza, “Je, umetia vitambaa hivyo mafuta?”

² Watu wengi huvitia mafuta, na ni sawa, Mungu hulibariki. Lakini kama mtayachunguza Maandiko, Paulo hakuvitia mafuta, bali alivitoa mwilini mwake. Mnaona? Kwa hiyo, tutaviombea sasa, nanyi mwombe pamoja nasi, kila mmoja. Na tuinamisha vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

³ Bwana wetu wa thamani, tumesimama hapa usiku wa leo katika vivuli vya rehema Yako, tukiomba kama kanisa la Mungu aliye hai kwa ajili ya vitambaa hivi vya thamani vilivyo hapa, lesa na vifurushi vidogo, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utawabariki, Baba, na jalia yeyote vitakavyowekwa juu yake, jalia Roho Mtakatifu aje juu yao, jalia waponywe, wakombolewe na kila mateso. Tunaweka mikono yetu kwa imani, kama ndugu na dada waaminio, kwa imani tunafanya hivi, tunapoomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁴ (Asante, ndugu.) Mnaweza kuketi. Ningetaka kusema hivi, kwamba nimekuwa na mikutano mingi Phoenix ambayo imeleta umati mkubwa zaidi, bali sijawahi kuwa na ukaaji wenye kufurahisha zaidi, na pamoja na ushirika, ambao umekuwa mmoja wa iliyo mikuu sana niliyowahi kuwa nayo.

⁵ Tumetembelea makanisa mbalimbali, tukaingia pamoja na Assemblies of God, na mara ya kwanza ninayokumbuka nilipopata kukutana kibinafsi, Ndugu Shores. Nami sisemi jambo hili, yeye akisimama hapa, lakini wakati unapoweza kusikia wahudumu wengine wa imani mbalimbali ambao wangeninii, si tu... imani ile ile, bali wa madhehebu mbalimbali, wakinena mema juu yake: mtu mwema. Hiyo ni kweli. Watu wengine ambao hawangekubaliana naye labda juu ya Mafundisho ya Biblia na mambo madogo madogo, wangepingana naye, na hata hivyo wanasema, “Ndugu Branham, huyo hapo mtu mtauwa.”

⁶ Kwa hiyo, tunashukuru kwa ajili ya ushirikiano wa Assemblies of God, kote mjini, Assemblies mbalimbali, na kadhalika. Bwana na awabariki sana.

⁷ Tulipokuwa hapa, na ikatubidi kutoka kwa Assemblies hapa, mbona sisi... Ni jambo la baina ya madhehebu. Halafu ninakuta kwamba kuna makundi mbalimbali. Nami nina furaha kwamba kuna makundi mbalimbali. Nina furaha kwamba Mungu hutufanya tofauti. Mungu ni Mungu wa vitu mbalimbali,

ana milima mikubwa na milima midogo, na Yeye ana—Yeye ana majangwa, na ana vinamasi, ana maua meupe, na maua ya samawati, na—na maua mekundu, halafu ana watu wadogo, watu wakubwa mno, wanawake wafupi, wanawake wanene, wanawake wakondefu, na loo, wote tu wa aina mbalimbali, Yeye ni Mungu wa namna mbalimbali. Wengine wenye nywele nyekundu, nywele nyeusi, baadhi ya wanaume wenye nywele za mawimbi, na wengine hawana hata kidogo. Na ninii tu, vema, Yeye ni Mungu wa namna mbalimbali, mnaona, Yeye hufanya tu mambo jinsi anavyotaka.

⁸ Hiyo ni kusema, jinsi ninavyowazia kuhusu... Yeye huwafanya watu weupe, watu wa hudhurungi, watu weusi, watu wa manjano, Mungu wa vitu vya namna mbalimbali. Mnaona? Nasi tuna tofauti za makanisa, tuna moja la namna *moja*, na moja la *nyingine*, bali sote tunaweza kuwa wanadamu pamoja. Mtu mweusi anaweza kumpa mzungu damu, kinyume chake, Mhindi anaweza kumpa mzungu, mzungu Mhindi, kwa kuwa “Mungu alifanya kutoka kwa damu moja mataifa yote.” Kwa hiyo alitufanya kuwa watu wamoja.

⁹ Lakini kama tu vile hekalu la Sulemani lilivyokatwa katika sehemu mbalimbali za nchi, lakini wakati yalipounganishwa, kulikuwa na aina mbalimbali za mawe, lakini ulipowadia wakati wa kuyaunganisha pamoja, yote yalingiana jiwe kwa jiwe, hakuna nyundo, hakuna misumeno, miaka arobaini katika ujenzi wake. Ninaamini wakati Mungu atakapokuwa tayari kulichukua Kanisa, hatutakuwa tukibishana kama sisi ni Wamethodisti, ama Wabaptisti, ama chochote tulicho, wote yataaungana tu.

¹⁰ Jumapili, juma lililopita, nilikuwa na ushirika mkubwa huko chini kwa Ndugu Fuller, Hekalu la Imani. Ndugu Fuller ni mtu mzuri sana. Anawakilisha wa—wale wasio na mipaka ya kimadhehebu. Ninii... kile wao... Ninaamini wanaitwa hivyo hapa, makanisa huru. Na yeye pamoja na Ndugu Groomer, hao, ni ndugu wanaojitegemea, kundi la watu wazuri sana, na Wakristo wazuri. Nimekuwa na makaribisho mazuri sana.

¹¹ Halafu basi leo, nilikuwa pamoja na Ndugu Outlaw, yule mtu aliyenifadhili mara ya kwanza nilipokuja Phoenix, yeye pamoja na Ndugu Garcia, watu wa Kimeksiko. Na huko juu kwenye... Ndugu Outlaw ana Maskani ya Jina la Yesu. Bila shaka tulikuwa na wakati mzuri sana pale asubuhi ya leo, Roho Mtakatifu alikuwa pale, nao walikuwa na kwaya iliyoimba. Nami ni—nina santuri zao kadhaa, nami kabisa siwezi kungojea kufika nyumbani na... Waliimba ule “Juu, Juu, Juu, Juu.” Ninaupenda huo.

¹² Mwajua, ni—nina Ukusini kidogo ndani yangu ambapo ninapenda kupiga makofi, mwajua, [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] mwajua, kwa namna fulani nihisi tu dini yangu.

Kwa hiyo, tulikuwa na wakati mzuri sana kule asubuhi ya leo katika ushirika pamoja na Ndugu yetu Outlaw. Bwana alikutana nasi kwa njia kuu. Na hivyo . . .

¹³ Anawakilisha United Pentecostal Church, na hao wengine wanawakilisha walio Huru, ndugu hapa ambaye huwakilisha Assemblies of God, nasi sote ni mmoja katika Kristo Yesu, sote tuna Roho Mtakatifu. Wakati mwingine, nitakaporudi, nitajaribu kuungana na makanisa mengine, yale ambayo sikuweza kukutana nayo. Kuwafanya tu mjue ya kwamba tunawapenda, haidhuru unaamini *nini*, ni *Yule* unayemwamini. Hilo ni zuri. Ni *Yule* unayemwamini. Nasi sote tunamwamini Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu wetu. Hatutumainii kazi zetu wenyewe wala ushirika wetu na kanisa, bali tunatumainia yale aliyotufanyia wakati alipokufa pale Kalvari.

¹⁴ Makundi makubwa, mazuri sana ya watu yamehudhuria hii mikutano. Watu hawa, wengi wao wamefunga makanisa yao wakati wa mkutano huu, tunawashukuru kwa ajili yake.

¹⁵ Wafanyabiashara Wakristo, hili tawi liliundwa katika kipindi hiki hapa, na—napenda hilo, nina furaha ilitukia nilipokuwa hapa. Mimi ninawaunga mkono Wafanyabiashara Wakristo, mradi tu wanaendelea kujitahidi hivyo kulisaidia Kanisa, si kuchukua mahali pa Kanisa, bali kulisaidia Kanisa kufanya ushirika na wafanyabiashara. Mbona, wafanyabiashara wanaweza kuwashuhudia wafanyabiashara. Ingekuwa, kama likiendelezwa hivyo jinsi limekuwa, litalijenga Kanisa, lilifanye kubwa zaidi. Tunashukuru kwa ajili ya chochote kinachoujenga Ufalme wa Mungu.

¹⁶ Na halafu ninataka kushukuru kila mmoja wenu kwa ushirikiano wenu mzuri, mkija usiku baada ya usiku. Hii imekuwa yapata siku kumi na tano za ibada na . . . mimi . . .

¹⁷ Mvulana wangu mdogo, Joseph, tuliposikia Indiana ina inchi kumi na nane za theluji mpya, yote hali ya hatari, na shule zote zilifungwa, na kadhalika, mvulana wangu mdogo, Joe, alisema “Baba, kwa nini hatuwezi kukaa siku mbili ama tatu, halafu tutaenda kwenye Mlima Kusini na kuwinda Gila wakubwa sana tena?” Mvulana mwerevu sana kwenye umri wa miaka minne.

¹⁸ Nikasema “Mpenzi, ningetaka kufanya hivyo, lakini kina dada hawana budi kurudi shuleni.” Halafu—halafu itatubidi kurudi moja kwa moja Tulsa pamoja na Ndugu Roberts na Ndugu Osborn, na nanii, ndugu wote kote nchini kwa ushirikiano mkamilifu. Ni ajabu jinsi watu wanavyokusanyika pamoja kwa njia hiyo, hilo ndilo nimeishi nipate kuona, kwamba ndugu wangeweza kuvuka ua. Jambo ndilo hilo, jambo ndilo hilo, jambo ndilo hilo, iweni ndugu.

Hatujagawanyika,
Sisi sote Mwili mmoja;
Mmoja katika tumaini na Mafundisho,

Mmoja katika upendo.

¹⁹ Huu “Twendeni, Askari Wakristo!” mashuhuri, hilo ndilo, hilo ndilo tunalotazamia, kule Kuja kwa Bwana Yesu.

²⁰ Sasa ninataka kuwashukuru ninyi nyote kwa ninii, ndio kwanza waniambie sasa hivi, Ndugu David na—na katibu wangu wa huduma, Bw. Mercier, ndiyo kwanza waniambie kwamba mlikuwa mmenipa matoleo mawili ya upendo ya mkutano huu. Asanteni, marafiki zangu wa thamani. Sadaka hiyo ya upendo itawekwa kwenye wakfu wa Maskani ya Branham, na itatumiwa kudhamini mikutano. Ninalipwa mshahara: dola mia moja kwa juma. Na kwa hiyo basi, hiyo itaenda kwa Ufalme wa Mungu.

²¹ Katika kila moja ya makanisa hayo, kwenye kanisa la Ndugu Outlaw asubuhi ya leo na huko chini kwenye kanisa la Ndugu Fuller Jumapili juma lililopita, nilijaribu kutowaruhusu kufanya hivyo, lakini walikuwa... yapata wakati nilipoingia mlango, Ndugu Fuller alikuwa ameweka hundi mkononi mwangu, kabisa ninasahau zilikuwa ngapi, yapata dola mia moja za umishenari. Na asubuhi ya leo, kanisa la Ndugu Outlaw lilitoa dola mia moja na moja na senti hamsini, matoleo ya umishenari. Katibu anayo, inaingia moja kwa moja kwenye wakfu kututuma ng'ambo kuhubiri Injili. Siku moja, ninaomba Mbinguni ya kwamba hiyo itakuwa saruji kwa ajili ya Makao yenu ya Milele Upande ule mwingine.

²² Tunawashukuru kwa ushirikiano wenu wote mwema, kwa kununua kweni kanda, kwa ajili ya vitabu na kadhalika. Navyo karibu vijishughulikie vyenye. Wakati mwingine inatubidi kuacha kampeni ivisaidie vitabu, kwa sababu kama hakuna mtu aliye na pesa nao wanataka kitabu, wanaweza kukichukua, kwa vyovyote vile, ni bure. Hiyo ni kweli. Silo wazo... Kusudi tu nipate za kutosha kuvichapisha tena vikaenezwe. Nasi... Wavulana hao hufanya kazi kwa mshahara mdogo sana kwa kuuza vitu hivyo, wanafanya kazi kote katika wakfu wa kanisa.

²³ Nalo kanisa... Kama unataka risiti za vitu hivyo, tuna namba sasa huko Washington, DC ambapo unaweza kupata rasmi ninii ya—yako, kupunguziwa kodi yako ya mapato, kutoka Washington, DC.

²⁴ Asanteni tena kwa kila kitu ambacho mmefanya, kwa ajili ya watu wazuri ambao wamekuwa mabawabu, na kusaidia katika mistari ya maombi, na zaidi ya yote, tunamshukuru Mungu kutoka kwenye kilindi cha moyo wetu, kila mmoja wetu, kwa ajili ya Uwepo Wake katika kila moja ya makanisa na hapa katika jumba hili la mikutano. Usiku baada ya usiku tumeona mkono Wake mkuu ukinyoshwa katika rehema kuwaponya wagonjwa, kuthibitisha kuonekana Kwake, na Kuja Kwake mara ya pili kukiwa kumekaribia.

²⁵ Ningetaka kuuliza usiku wa leo, wakati jumba la mikutano likiwa karibu limejaa, nafikiri, usiku wa leo, uwanja huu,

kwamba ningewaomba ninyi nyote mniombee. Huenda ikawa, katika siku chache zijazo, juma moja, au majuma matatu au manne au matano, kwamba mimi na Ndugu du Plessis tutaenda Ulaya, kote Ulaya, katika mikutano. Labda baadaye kidogo katika msimu wa kiangazi, tutashuka kwenda Australia, New Zealand.

²⁶ Na halafu ilikuwa ni kwa Wafanyabiashara Wakristo wanaotaka siku thelathini huko (Hilo jina lilikuwa gani?) [Ndugu mmoja anasema, “Kuba.”—Mh.] Kuba, ambako serikali inatualika kuja, na Haiti, na sehemu hizo huko ndani. Na halafu pia, mahali tulipokuwa, huko chini katika Visiwa vya Karibea na Pueto Riko, kundi lile lile lililomdhamini Billy Graham lilikutana nami kule na linataka kisiwa kizima, kufanya m—mzunguko wa mzingo wa moto kote, usiku katika sehemu *hii*, usiku katika sehemu *ile*, kisha turudi kwenye uwanja wa mpira tena kwa ajili ya mkutano mkubwa katika uwanja wa mpira. Sifa kuu walizotoa kuhusu huo mkutano, na kadhalika! Loo, mavuno kweli yameiva, watenda kazi ni wachache. Na tumwombe Bwana kwamba . . .

²⁷ Ninataka kuzishukuru nyumba ninazotembelea kwa kuwa wazuri sana, hasa Ndugu na Dada Sharrit, na Ndugu na Dada Williams, na ushirika wote mzuri, kila mahali, hakika tunawathamini kwa mioyo yetu yote. Ninasema hivyo kwa ajili ya mke wangu, familia yangu, mwanangu, Ndugu David du Plessis, Ndugu Roy Borders, mwenzangu, Ndugu Gene Goad, na Ndugu Leo Mercier, wafanyakazi wote, Ndugu Sothmann, Fred Sothmann kutoka Kanada, ambao pia ni wahudumu kanisani, ni mmoja wa wadhamini katika hilo shirika. Tunawashukuru ninyi nyote kwa hayo, kutoka miyoni mwetu. Mungu awe pamoja nanyi, nasi tunatumaini kurudi pamoja nanyi tena kabla Yesu hajaja ikiwezekana. Mungu awabariki, ayafanikishe makanisa yenu, na watu wengi waokolewe.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

²⁸ Sasa Baba wa Mbinguni, hakika kabisa tunataka kukushukuru, kwa kuwa imekuwa ni Neema Yako ambayo imetufanyia haya yote. Tumefanya hivyo, Bwana, tukija hapa kufanya ushirika pamoja na makanisa, pamoja na ndugu, kukutana na hawa watu wa thamani tena. Tunajisikia kama Paulo alivyojisikia wakati huo walipomfuata mpaka ufukoni mwa bahari nao wakapiga magoti na kuomba.

²⁹ Bwana, Roho yuyo huyo anaishi ndani ya wanaume na wanawake mumu humu Phoenix. Na wakati tunapowaona, na kufanya ushirika tena, na kuzungumza juu Yako pamoja na kuja Kwako, na kulihubiri Neno, na kuona watoto Wako wagonjwa wakisaidiwa, makanisa yakijengwa pamoja na kuingia kwa

wafuasi wapya, tunakushukuru sana, Bwana. Imekuwa ninii . . . Neema ya ajabu!

³⁰ Tunaomba ya kwamba utalibariki jiji hili na wahudumu wake wote, na jalia Kanisa likue na kufanikiwa kupitia Yesu Kristo.

³¹ Sasa, tunalijia Neno, kwenye maneno ya mwisho ya uamsho huu. Baba Mungu, tunakutaka uwe na Maneno ya mwisho. Tunataka kuhisi baraka Zako juu yetu, kuisikia Sauti Yako ikisema nasi tena usiku wa leo. Na tunapojitahidi kusoma Neno Lako tukufu na takatifu lililovuviwa, tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atayachukua hayo Maneno na kuyagawanya, kwa kila mmoja, mioyoni jinsi anavyotaka na mahali yanapohitajika. Jalia Mbegu ianguke kwenye udongo wenye rutuba, ikue ikawa Miti mikuu ya wokovu. Tujalie, Bwana.

³² Tubariki na utusaidie tunapoendelea kuingia katika ibada. Katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, wa thamani, Bwana Yesu, tunaomba. Amina.

³³ Ningependa kufungua usiku wa leo kwenye Mathayo mlango wa 17, kusoma kwa muda kidogo tu, vifungu vichache. Wakati mkifungua, ningetaka kuwaambia wasikilizaji, pia, kwamba ninathamini pongezi zenu kwa mwenzangu, Ndugu David du Plessis, mambo mazuri ambayo nimeambiwa kuhusu kufundisha kwake. Ninawashukuru nyote kwa pongezi zenu. Nina hakika yatawanufaisha.

³⁴ Sasa, mlango wa 17 wa Injili ya Mathayo Mtakatifu, kuanzia kifungu cha kwanza:

Na baada ya siku sita Yesu awatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani.

Akageuka sura mbele yao: uso wake ukang'aa kama jua, . . . mavazi yake yakawa meupe kama nuru.

Na, tazama, wakatokewa na Musa na Eliya wakizungumza naye.

Petro akajibu, akamwambia Yesu, Bwana, ni vizuri sisi kuwapo hapa: ukitaka, na tufanye hapa vibanda vitatu; kimoja chako wewe, . . . kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya.

Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli: na . . . sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.

³⁵ Ninataka kuchukua maneno hayo matatu ya mwisho kwa ajili ya somo: *Msikieni Yeye*. [Kiingereza: *Hear Ye Him—Mfa.*] Ninarudi tena usiku wa leo na fungu dogo sana kwa ajili ya kusanyiko kama hili, maneno matatu. Lakini hayo ni . . . Kama

tunaweza kuyatii maneno hayo matatu usiku wa leo, utaona kurudiwa kwa Pentekoste katika jengo hili. Ni madogo tu, lakini, loo, kuna nguvu za kutosha hapo ndani, hata Biblia nzima itaungana nayo: *Msikieni Yeye*. Si maneno mengi mno.

³⁶ Wakati mwingine tumewapata ndugu wa hii imani ya thamani, nami nimesikia hili mimi mwenyewe, wakati wangesema, “Loo, Ndugu Branham, siamini ina faida yoyote kwangu kuendelea mbele zaidi. Nilikuwa kule kumsikia Billy Graham, na, loo, kulikuwako na maelfu *mengi sana* ya watu. Kisha nilikuwa huko nje kumsikiliza ndugu yetu mheshimiwa sana, Oral Roberts, na maelfu ya watu walijaa hemani, kwa hiyo inaonekana tu kana kwamba labda umati wangu mdogo hauna maana sana.”

³⁷ Lakini mmekosea sana. Hivi unathamini kidole chako? Usingetaka kidole chako kiseme, “Kwa sababu mimi si jicho wala sikio, sitafanya kazi tena.” Ni tofauti sana.

³⁸ Inanikumbusha hadithi ndogo wakati mmoja wakati marehemu Mfalme George alipokuja kufanya ziara Canada, yeye na mke wake wa thamani. Mfalme alikuwa akiugua wakati huo ugonjwa wa kukakamaa kwa mwili, ambao alikuwa amesema kwa simu baadaye, nami nilikuwa na majaliwa ya kumwombea, nilipopata barua kutoka kwake. Basi ile siku ambayo alikuwa apitie Vancouver, British Columbia, alikuwa ameketi kwenye gari lake la kibandawazi alipokuwa akiendesha barabarani, na watu wote wakaziachilia shule, waalimu, nao wakajiandaa kumlaki mfalme na kuwa na wakati mzuri sana.

³⁹ Ninamkumbuka mwenzangu, Ndugu Ern Baxter, Ndugu Baxter akasema, “Ndugu Branham, niliposimama pale na kumwona mfalme akipita, naye mke wake mpendwa amevaa nguo yake maridadi ya samawati,” kasema, “nilicheka kichinichini tu na kulia.”

⁴⁰ Mnaona, ilimaanisha jambo fulani kwake, huyo alikuwa ni mfalme na malkia wakipita. Nami nikawazia, “Kama kumwona mfalme wa Uingereza akipita, watu wa Canada,” ambao ni sehemu ya raia wake, “kama wanguweza kujisikia hivyo, na mhemuko ungeinuka kumwona mfalme wa Uingereza akipita, itakuwaje wakati Mfalme wa Utukufu atakapopita?”

⁴¹ Watoto wote wadogo walipewa bendera ndogo ya Uingereza, ndipo wakati mfalme alipopita, iliwapasa kupeperusha bendera hii ndogo, na—na kuimba, *Mungu Mlinde Mfalme* wakati ukipita. Basi wakati ulipowadia, mfalme alipokuwa amepita mtaani na kuingia hotelini mwake, ama popote alipotarajiwa kukaa, watoto walikuwa warudi shuleni.

⁴² Basi katika shule fulani wote walirudi isipokuwa msichana mmoja mdogo. Naye mwalimu akafadhaishwa sana na jambo hilo, akatoka akaenda mitaani kumtafuta jamaa huyo mdogo, naye akamwona maskini msichana huyu amesimama karibu na

nguzo ya simu, ameiegemea, huku akilia kwa moyo wake wote. Na kwa hiyo, akamkimbilia maskini msichana huyo, mdogo wa kimo, akamchukua, naye alikuwa akilia kana kwamba maskini moyo wake ungevunjika. Naye akasema, “Unalia nini, mpenzi? Kwani hukumwona mfalme?”

Akasema, “Naam, nilimwona.”

Vema, kasema, “Je, ulipeperusha bendera yako ya uzalendo wakati akipita?”

Akasema, “Nilimpeperushia mfalme bendera yangu wakati akipita.”

“Na ulimwona?”

“Naam, nilimwona.”

Kisha akasema, “Kwa nini unalia?”

Akasema, “Mwalimu, nilimwona mfalme, lakini mimi ni mdogo sana mfalme hakuniona.”

⁴³ Hivyo sivyo ilivyo kwa Yesu. Haidhuru unafanya kidogo jinsi gani, Yeye anajua kila kitu unachofanya. Imerekodiwa Mbinguni kwenye akaunti yako sawasawa na ya Billy Graham, ama ya Oral Roberts, ama yeyote wa hao wengine walio na mikutano mikubwa. Si mambo makubwa wakati mwingine tunayoyafanya, ni mambo madogo tunayoacha bila kufanya.

⁴⁴ Sasa, Yesu hayaheshimu makundi, Yesu alikutana katika makundi ya kila namna, ukubwa wote, na matabaka yote ya maisha. Wakati mmoja tuna kumbukumbu Yake akikutana na mia tano, wakati mwingine na maelfu, wakati mmoja tunamwona akiwa na kumi na wawili, wakati mwingine, wakati tunamwona nao mlimani. Si kanisa takatifu, si watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya watu anayelifanya *kitu fulani*. Si kanisa, wala watu, ni Roho Mtakatifu.

⁴⁵ Bila shaka hili lilikuwa ni tukio maalum, tukio kuu. Petro aliuita baadaye, “mlima mtakatifu.” Sasa, siamini ya kwamba Petro alimaanisha ya kwamba huo mlima ulikuwa mtakatifu, ninaamini Petro alimaanisha ya kwamba Mungu Mtakatifu alikutana nao mlimani. Si kanisa takatifu, si watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya watu anayelifanya *kitu fulani*. Si kanisa, wala watu, ni Roho Mtakatifu.

⁴⁶ Mungu anapoanza kufanya jambo lolote kubwa, kwa kawaida Yeye hulitangaza kwanza mbinguni. Na hili hapana shaka lilikuwa ni tukio maalum, walikuwa wakipanda kwenda kwenye ule tunaquita Mlima wa Kugeuka Sura. Naye alikuwa amesema siku chache hapo kabla, “Amin, nawaambia, wapo wengine waliosimama hapa ambao hawataona mauti hata watakapomwona Mwana wa . . . Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu.”

47 Ninaamini, kama labda wahudumu wote, ama wengi wao, wanajua ya kwamba mandhari hii ilimaanisha kule Kuja... utaratibu wa Kuja kwa Kristo. Jambo la kwanza waliloona, na jinsi huo utaratibu ulivyokuwa, walimwona Yesu, ambaye alikuwa atokee, kisha wakaona kule kuja kwa kutukuzwa, na Musa, na Eliya, utaratibu wenyewe wa Kuja mara ya pili, ndipo walipoangalia nyuma, walimwona Yesu pekee, walipoangalia tena.

48 Sasa, tunaona ya kwamba Yeye aliwapeleka kule juu kwa kusudi fulani, Naye akawachukua watatu. Katika Agano la Kale, pia lile Jipya, tatu ni thibitisho, "Kwa vinywa vya mashahidi wawili watatu, kila neno na lithibitike." Hiyo ni katika Agano la Kale, na pia katika Agano Jipya. Nasi tunaona ya kwamba Yesu aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana, mashahidi watatu wa duniani kushuhudia; naye Mungu alikuwa nao mlimani, Musa, Eliya, na Yesu, kama ushuhuda wa Mbinguni. Mungu alikuwa akijiandaa kufanya jambo kubwa.

49 Yale ninayofikiri ya kwamba Mungu alikuwa akifanya hapa, moja ya mambo ambayo ningetaka kuwakumbusha, ninaamini ya kwamba Mungu alikuwa akijaribu kuweka, ama, kufuata sheria Zake Mwenyewe. Mungu hana budi kufuata sheria Zake Mwenyewe, hana budi kuishi katika sheria Zake Mwenyewe.

50 Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba Yesu alikuwa ni zaidi ya nabii, Yesu alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili. Mungu asingeweza kumtuma mtu mwingine aliyezaliwa na mwanamume na mwanamke kuchukua mahali hapo na kuwa, kuchukua... kumeza mauti, kwa sababu ilimbidi Mungu kuchukua adhabu Yake Mwenyewe. Mungu asingeweza kufa katika Roho, kwa hiyo alifanyika mwili akakaa kwetu kusudi apate kufa, nayo hukumu yetu iliwekwa juu ya mwili Wake wa thamani ndipo akafa kwa ajili yetu sote.

51 Pale katika mwili huo wa thamani, unaoketi mkono Wake wa kuume wa Ukuu usiku wa leo. Mungu hawezi kuangalia maradhi tena, yamehukumiwa. Hawezi kuiangalia dhambi tena, imehukumiwa. Huo hapo ule Upatanisho umeketi, mwili wa Bwana Yesu uliochubuliwa kisha ukapigwa, umeketi kwenye mkono Wake wa kuume Mbinguni. Hilo ndilo linalotufanya tuwe na imani, kwa sababu Yeye ameketi pale apate kutuombea tunapokiri.

52 Mungu pia hapa alikuwa akifanya kile tunachoita katika Biblia, kufanywa mwana mwenye mamlaka. Sasa, katika Agano la Kale wakati mtoto alipozaliwa, mwana nyumbani, basi mwana huyo alikuwa ni mwana mara tu alipozaliwa, bila shaka, alikuwa mwana wa huyo baba. Lakini hata hivyo kabla hajarithi ufalme wa baba yake, ama milki yake, kwanza ilibidi mwana huyo alelewe na kujaribiwa. Ilimbidi achunguze kama mwana huyu alikuwa ni mwana wa kweli, au alikuwa

tu ni mzururaji. Wala mwana huyu asingekuwa mrithi kama hakustahili kuchukua mahali pa baba yake, lakini kama alistahili na kuchukua mahali pa baba, basi yote aliyokuwa nayo baba alipewa mwanawe.

⁵³ Hapo ndipo ninapowazia ya kwamba wengi wetu Wapentekoste tumekosea. Tunawazia mara tu tunapofanyika wana na binti za Mungu, hilo latosha, tunafikia tu mahali pa kujaribiwa. Wamethodisti walisema mara walipopaza sauti, hilo lilitosha; Walutheri walianini kwa imani juu ya kuhesabiwa haki nao wakawazia hiyo ilitosha, haidhuru Mungu amekuweka katika nafasi ya namna gani, ungali unakuwa, ukielekea kwenye ukamilifu, na kamwe hatutaufikia mpaka Yesu atakapokuja.

⁵⁴ Sasa, katika Agano la Kale, Mungu alikuwa na ufalme Wake wa watu wanaoendelezwa kama tu walio Wake Mwenyewe chini ya sheria za kale. Sasa, baba mmoja alikuwa na eneo la ardhi, alikuwa na mikono ya kukodiwa na wote huko kwenye ardhi hiyo.

⁵⁵ Tunaona katika Toleo la King James katika Yohana 14, tunasoma pale, ilisema, “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi.” Hilo linasikika la kigeni, sivyo? Majumba makubwa katika nyumba moja. Sijui kama ni Moffatt, mmojawapo niliyekuwa nikisoma, wa wafasiri, aliifanya ya kuchekesha kuliko hiyo, kasema “Nyumbani mwa Baba Yangu mna vyumba vingi,” kama kwamba tulikuwa tukienda kule kuchukua vyumba vya kukodisha. La, hayo yote ni makosa.

⁵⁶ Basi katika siku za wafasiri wa Toleo la King James, ndivyo ninavyoambiwa, kwamba walitafsiri katika lugha ya siku hizo, sasa, huko Uingereza, kweli, mfalme alikuwa ndiye baba, na milki yake yote ilikuwa nyumba yake. Hiyo inapatana kabisa na Agano la Kale, kwamba baba alikuwa, alikuwa na milki yake, naye alikuwa ndiye mtawala katika milki hii.

⁵⁷ Na mara huyo mtoto alipozaliwa, baba akiwa na shughuli nyingi sana na mambo mengine, alitafuta mwalimu, au mlezi, wa mtoto wake. Halafu basi, yeye akijua ya kwamba mtoto huyu alikuwa katika mstari wa mrithi wa kila kitu alichokuwa nacho, mali yake, jina lake zuri, na kila kitu alichokuwa nacho kingemwendea mwana huyu, alitafuta mwalimu bora sana wa shule ambaye angeweza kumpata kumfundisha mtoto huyo.

⁵⁸ Naye Mungu hufanya vivyo hivyo kwa watoto Wake. Mtu anapozaliwa katika Mwili wa Bwana Yesu, na kufanyika mwana wa Mungu, Mungu ametafuta Mbinguni apate Mwalimu aliye bora zaidi amjuaye kumweka juu ya watoto Wake. Wala si askofu, bali ilikuwa ni Roho Mtakatifu, Mungu aliweka juu ya Kanisa Lake kuliinua Kanisa Lake liamini mambo ya kiroho na matendo ya kimbinguni ya Mungu. Asingeweka askofu juu ya Kanisa Lake ambaye haamini katika siku za... anayeamini siku za miujiza zimepita, na mambo yote ya kimbinguni

yamekwisha; Mungu asingefanya hivyo. Naye Roho Mtakatifu alitumwa kulitawala na kuliongoza Kanisa. Mungu alimpa Roho Mtakatifu kufanya jambo hili.

⁵⁹ Baba asingetafuta mtu ambaye angejaribu kujigamba, kama tusemavyo, na kusema, “Vema sasa, yeye ataninii... anajua mimi ndiye baba, kwa hiyo ataninii, huyo mwana, maskini haini, kitu kama hicho, lakini angekuja, na, kujitakia makuu, ‘Loo, mwanao anaendelea vizuri sana.’” Asingefanya hivyo. Alichukua mtu ambaye angemwambia ukweli, kwa kuwa alitaka kujua masilahi ya mvulana huyo wakati wote.

⁶⁰ Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Yeye kamwe hakuliaminisha kwa papa yeyote, askofu, ama chochote kile, Alilituma Roho Mtakatifu juu ya Kanisa awe Mwalimu na Mlezi wa Kanisa. Kwa hiyo, Roho Mtakatifu atakuwa mwaminifu kwa Mungu.

⁶¹ Na sasa mlezi huyu, mwalimu huyu, alipaswa kuja na kumjulisha baba, jinsi mtoto huyo alivyokuwa anaendelea. Na jinsi ambavyo hapana shaka huyo mwalimu aliona haya kama mtoto huyo alikuwa akienenda vibaya, jinsi ambavyo hu—huyo mvulana mdogo hakuvutiwa na mambo ya shamba au ufalme wa baba yake.

⁶² Jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hana budi kujisikia leo, anapoenda mbele za Mungu akiwa na uso wenye aibu, ulioinamishwa tuseme, kulazimika kupeleka ripoti ya kutokujali kwetu kanisani leo! Jinsi ambavyo tumeweka kando ubatizo wote wa Roho, jinsi ambavyo makanisa yana mfano wa utauwa na kukana nguvu zake. Jinsi ambavyo hana budi kuona haya kusema, “Binti zako wanavalia kizinifu.” Jinsi ambavyo hana budi kuona haya kusema, “Watoto wako hata hawawezi kukubaliana kwa muda wa kutosha kufanya mkutano. Jinsi ambavyo wanawadhihaki watu Wako ambao wameitwa watoke na kujazwa na Roho.” Jinsi Roho Mtakatifu hana budi kujisikia kwenda mbele za Mungu na jumbe kama hizo!

⁶³ Akirudi, akisema, “Wana mfano wa utauwa... Hawaamini mambo ya kimbinguni tena. Hata hawataenda kanisani Jumatano usiku, wanakaa kutazama kipindi wanachokipenda cha televisheni.” Jinsi haina budi kuwa!

⁶⁴ “Na karama Zako unazotuma kwa Kanisa Lako kulithibitisha Neno Lako uliloahidi, watu wanaondoka na kuziita kazi za ibilisi.” Sasa kumbukeni, Roho Mtakatifu hana budi kumletea Mungu kila kitu ambacho kila mtu anayekiri kuwa Mkristo anasema juu yake. Kwa sababu Yeye alituma...

Vema, naomba Baba aseme, “Ulijaribu? Je, ulibisha mlango wa moyo?”

⁶⁵ “Nilibisha usiku baada ya usiku, nao hawatasikiliza.” Jinsi hana budi kujisikia! Inawezaje...? Alituamini. Kama alivyowafanyia Adamu na Hawa, akawaweka katika bustani

ya Edeni na akatumainia watakuwa sawa, kulitii Neno Lake, wakaanguka. Na mara mwanadamu anaposhika vitu mkononi mwake, ataanguka kila wakati, hawezi kuvishikilia mwenyewe, inahitaji Mungu kutushikilia.

⁶⁶ Ndipo tunaona tena, ya kwamba wakati... Vipi kama mvulana huyo alikuwa ni mvulana mzuri? Loo, jinsi mwalimu angetokeza kifua chake, aende kwa baba, na kusema, "Nina furaha sana, bwana, kukuletea ujumbe wa jinsi mwanao anavyoendelea. Yeye ni mwerevu tu awezavyo kuwa, yeye ni kama tu—kama tu wewe. Yeye ni, kama tunavyoweza kumwita, mtoto anayefanana na babaye kabisa. Yeye ni kama wewe kabisa, anapenda kitu kile kile unachopenda. Yeye hufanya kazi kama vile ulivyoifanya ulipokuwa huko nje."

⁶⁷ Hiyo ndiyo aina ya kanisa ambalo Roho Mtakatifu anapenda kulishuhudia mbele za Mungu. "Aina ya kazi," Yesu alisema, "nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya." Hiyo ndiyo aina ya kanisa ambalo Roho Mtakatifu anapenda kushuhudia mbele za Mungu.

⁶⁸ Ndipo basi kama mtoto huyo, huyo mwana, hakutii wala hakuwa mtoto mtiifu, kamwe hakuwa zaidi ya mwana, alibaki mwana, bali hata hivyo hakuwa na urithi.

⁶⁹ Sasa, hatutaki kukaa mahali hapo. Kanisa linapaswa kuwa maili elfu moja juu barabarani kuliko lilivyo usiku wa leo. Baraka za Kipentekoste zimekuwa zikiwashukia watu hapa Marekani kwa muda wa miaka hamsini, na kama kuna chochote, tunafifia, badala ya kuendelea.

⁷⁰ "Kwa nini unahubiri jambo kama hili, Ndugu Branham?"

⁷¹ Ninataka kuona Kanisa la Mungu katika uaminifu mkubwa, ninataka kuona mikutano ya maombi ya mtindo wa kale. Ninataka kuona zile nyakati ambapo hawawezi kuondoka kanisani, wanakesha tu usiku kucha, na kuomba, na kufunga, na kuita mpaka Mungu ajibu, badala yake, inaonekana kana kwamba upendo umefifia kutoka kwetu. Upendo wa Mungu, upendo tu...

⁷² Mbona, Mkristo halisi ni vigumu kungojea, wakati kengele inapolia, amechukua kiti cha mbele, na hapo tayari na kitabu cha nyimbo mkononi mwake. Lakini sasa, tunasema, "Loo, jamani, sijui."

Loo, kibarikiwe kifungo kiifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa Juu.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana katika moyo,
Na kutumaini kukutana tena.

Hivyo ndivyo Ukristo halisi ulivyo tukio lililo hai.

⁷³ Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio ambalo mtu yeyote anaweza kuwa nalo kama watataka kuwa nalo. Ni jambo fulani unalopitia, Roho Mtakatifu.

⁷⁴ Sasa, wakati mvulana huyu, kama alikuja namna hiyo wala hakuwa mtiifu, hakuwa na tendo la baba yake, hakujaribu kuendeleza shughuli za baba yake jinsi baba yake alivyofanya, basi mtoto huyo alikosa urithi wake wote, ilimbidi ndugu mwingine kuchukua mahali pake.

⁷⁵ Sasa, siku hizi kama tukijaribu kulipeleka Kanisa mbele za Mungu chini ya kanuni za kawaida tu za kanisa ama theolojia, hivyo sivyo Yesu alivyolipeleka Kanisa mbele za Baba. Mungu analitaka Kanisa lijazwe na Roho Mtakatifu, likifanya kazi zile zile alizofanya Yeye alipokuwa hapa duniani. Hiyo ndiyo aina ya Kanisa ambalo Mwalimu, Roho Mtakatifu, atataka kuliwasilisha mbele za Mungu.

⁷⁶ Kama nilivyowaambia wakati mmoja hapa, ule mkataba ambao, katika Agano la Kale, wakati ulipoandikwa kisha ukapasuliwa vipande, vilipokutana, ilibidi viumane, ilibidi kila kipande cha karatasi kiumane moja kwa moja, na mpango wote ulingane kabisa. Mungu alithibitisha agano Lake na watu kupitia kwa Isaka hadi kwa Kristo, na pale Kalvari Yeye alimrarua Masihi vipande. Aliuchukua huo mwili na kuuweka mkono Wake wa kuume, kisha akamtuma Roho hapa chini juu ya Kanisa. Nalo Kanisa litalazimika kuwa na Roho yeye yule, likifanya mambo yale yale aliyofanya Yesu, la sivyo kamwe halitanyakuliwa. Kushikamana.

⁷⁷ Chukua kipande hiki cha karatasi hapa ukipasue. [Ndugu Branham anararua kipande cha karatasi—Mh.] Sasa, usingeweza kukiigiza hata ufanye nini. Hakina budi kirudi karatasi ile ile, ili kwamba herufi hizo zirudi jinsi tu zilivyokuwa. Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa hasa. Yesu sikuzote alikuwa kwenye shughuli ya Baba, akifanya yale yaliyokuwa mema machoni Pake, sio tu kuhusu kufanya *hivi* na *vile*, yale yanayopendeza kanisa kufanya, bali ni kufanya shughuli ya Baba, naye Yesu alikuwa na ushuhuda, “Sikuzote mimi hufanya yale yanayompendeza Baba.”

⁷⁸ Ule mfano, Henoko, kabla ya kule kuhamishwa, Henoko alitembea pamoja na Mungu miaka mia tano, na alikuwa na ushuhuda ya kwamba alimpendeza Mungu. Naye alikuwa ni mfano wa Kanisa lililonyakuliwa. Loo, tumepungukiwa.

⁷⁹ Ndipo mtoto huyo, ilimbidi Mungu kumwinua mtoto mwingine. Na kama Pentekoste ikimpungukia Mungu, Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Mungu anaweza kuwaita kutoka kwa Walutheri, kutoka kwa Wabaptisti, kutoka kwa Wapresbiteri, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Mtu fulani atalionga hilo ono na kuliendeleza.

⁸⁰ Sikusudii kuwaziba masikio wala kuwatisha watoto wachanga, lakini ninapata tu mvuke mwingi, nami sina budi kuupulizia mahali fulani, unaongezeka. Ninajisikia vizuri, ninajisikia kubarikiwa, maana ninajua ya kwamba Roho Mtakatifu yeye yule aliyeliandika Neno yupo hapa akilithibitisha Neno kwa Neno, herufi kwa herufi, “kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo. Na ushikilie sana yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo Raha, Sabato. Haya yote wasingeweza kuyasikia. Kwa maana Neno huja herufi kwa herufi, kanuni juu ya kanuni.”

⁸¹ Sasa, kama mtoto huyo wakati huo hakutii, hakuwa kwenye shughuli ya Baba, Mungu angeninii, angeweza kumwinua mwana mwingine. Hivyo ndivyo amefanya katika nyakati zote, kumwinua Luther, kumwinua Mmethodisti, kumwinua Mnazarayo, kumwinua Mplgrim Holiness, kumwinua Mpentekoste, ataendelea kuwainua, na kuwainua, na kuwainua mpaka atakapompata mmoja. Haleluya!

⁸² Mungu, ninatumaini kuishi kuona Kanisa hilo litakapoinuka katika nguvu na uzuri wa ufufuo, huku nguvu za Mungu zikitenda kazi kupitia Kwake, ishara na maajabu yakiwafuata waaminio kama ilivyokuwa katika A—Agano Jipya. Mungu katika nguvu Zake na katika uweza Wake! Loo, ni ajabu jinsi gani!

⁸³ Basi kama Kanisa hili lilitii, jinsi yule Mwalimu alivyopenda kumjia Baba, na kusema, “Loo, yeye ni mzuri sana! Mbona Wewe...Kazi imefanywa jinsi hasa Wewe ulivyoifanya.” Mnapata ninalomaanisha? “Huyo Mwanao kule chini, Baba, anafanya kazi, maagizo Yako herufi kwa herufi tu, jinsi Wewe ulivyoifanya.” Hiyo ndiyo aina ya Kanisa, hilo Ndilo.

⁸⁴ Basi jinsi baba anavyosema, “Hakika ninajivunia huyo mwana!” Mnajua kinachotukia? Wakati anapopata elimu yake, mafunzo yake, hata hivyo huenda asiweze kutumia mamlaka yote, bado hajayapata, angali ni mwana, bali hajawekwa mahali pake. Sasa, ninyi wahudumu mnajua mahali nilipo, kile ninachoendea: kufanywa mwana mwenye mamlaka.

⁸⁵ Sasa, kama mwana huyo alithibitika kuwa mwana mzuri, alipenda shughuli za baba, alidumu moja kwa moja na maagizo yake, basi baba siku moja alimpeleka mwana huyo mbele ya umma, akampandisha mahali pa juu, akamvika vazi la kupendeza, naye akafanya kile wanachoita kufanywa mwana mwenye mamlaka, ama kuweka mwana, mahali pake, kile alichokuwa.

⁸⁶ Walifanya sherehe, ndipo baba akasema, “Huyu, mwanangu, ninamfanya mwana mwenye mamlaka, ama ninamweka mahali pake.” Na kama walikuwa na hundi siku hizo, jina la mwana huyo kwenye hundi lilikuwa sawa tu na vile jina la baba

yake lilivyokuwa, maana aliwekwa mahali pake. Naye huyo mwana angeweza kumfukuza kazi yule aliyetaka, angeweza kumwajiri yule aliyetaka, alimiliki kikamilifu mali yote baba yake aliyokuwa nayo.

⁸⁷ Sasa, mnaona, Yesu alikuwa amemthibitishia Mungu ya kwamba Yeye alikuwa Mwana sahihi. Ndipo Mungu akampandisha juu ya mlima, akaleta mashahidi huko nje, mashahidi wa Mbinguni na mashahidi wa duniani, ndipo Yeye akamvika kutokupatikana na mauti. Walipoangalia juu, walisema, “Mavazi yake yaling’aa kama jua.” Jambo fulani la kimbinguni lilitukia. Mavazi yake yaling’aa kama jua wakati wa mchana, meupe yalivyoweza kuwa. Mungu aliweka juu Yake vazi hilo la kutopatikana na mauti, akionyesha ya kwamba alikuwa amempokea.

⁸⁸ Hilo ndilo jambo ambalo Mungu atawafanyia wanawe hapa duniani, siku moja. Atawaita kando, enyi Kanisa, kama tu mtamtii Yeye, na kudumu kwenye Neno na kuliadini. Naye ataweka Kanisani, kabla ya kuja kwa Yesu Kristo, ataweka Kanisani, nguvu zote ambazo Kristo alikuwa nazo ndani Yake zitakuwa ndani ya Kanisa.

⁸⁹ Yote aliyokuwa Mungu, aliyamwaga ndani ya Yesu, yote aliyokuwa Yesu, anayamwaga ndani ya Kanisa. Mungu akitaka kazi Yake ifanywe, aliituma katika Mwanawe, Mwana akitaka kazi ifanywe, aliituma Kanisani. “Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Siku hiyo, kwa sababu nguvu zile zile za Mungu, zilizokuwamo katika Yehova Mungu, zilikaa katika Yesu Kristo, nguvu zile zile zilizokaa katika Yesu Kristo, zinakaa katika wana waliwekwa mahali pao katika Mwili wa Kristo.

⁹⁰ Kumweka mwana mahali pake, kumpeleka nje mahali fulani, kufanya sherehe mbele za Malaika, na kumweka mahali pake kile alichokwa katika Mwili wa Kristo, basi mtu huyo ana mamlaka.

⁹¹ Hebu niseme jambo hili, hata mkinihesabu mimi kuwa mshupavu wa dini tangu usiku huu na kuendelea: Jambo lilo hilo ninalozungumzia litatimia. Kutakuwako na nguvu zitakazowekwa Kanisani, na sasa zinaingia, kwamba Roho Mtakatifu atawatia watu mafuta sana, hata watanena neno, nalo litajiumba lenyewe papo hapo. Hatujaona nguvu kama zile zinazolingia Kanisani sasa. Ninajua hilo kuwa ni kweli.

⁹² “Ukiuambia mlima huu ng’oka, usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Kuwekwa kwa Kanisa mahali pake, ambapo utimilifu wa nguvu za Roho Mtakatifu unakuja Kanisani. Ndipo vinywa vya wakosoaji vitafungwa. Itakuwa ni muda mfupi; Yesu aliposhuka moja kwa moja kutoka mlimani, alienda moja kwa

moja mpaka Kalvari. Angalieni, hautadumu muda mrefu, bali utakuwa hapa.

⁹³ Sasa, wakati mambo ya kimbinguni yanapofanywa katika kuwekwa wakfu...Wakati mambo ya kimbinguni yanapofanywa, yanawasisimua watu, yanawafanya wote washikwe na msisimko na kuingia wazimu. Wakati Musa alipofanya mambo ya kimbinguni huko chini Misri, kulikuwako na kundi la watu waliochanganyikana walioenda pamoja nao, wakasababisha vurugu kambini. Mnajua hilo, wasomaji wote wa Biblia wanajua jambo hilo. Ilisababisha kundi lililochanganyikana mno, waaminio waliochanganyikana na wasioamini, ilisababisha vurugu kambini baadaye. Wakati mambo ya kimbinguni yanapofanywa, huwafanya watu wasisimkwe, nao wanaenda kombo.

⁹⁴ Hilo ni jambo lile lile lililotukia katika milki yenu ya Kipentekoste. Mambo ya kimbinguni yalifanyika. Mungu alimwaga kitu cha kwanza, Kipawa cha Roho Mtakatifu kuwaacha watu wanene kwa lugha. Ndipo wakapata uigaji mwingi sana kwake, kujilinganisha kimwili. Watu wanashuka na kurudia neno moja tena, na tena, na tena, na tena, mpaka wanapata namna fulani ya lugha ya kunena, ama mambo ya kimbinguni kwa njia yoyote yanaanza kufanywa, ndipo kuna mtu anayejaribu kuyaigiza.

⁹⁵ Je, mnajua Mungu kamwe hakuwaumba watu wawili namna ile ile? Hakuna wawili wenu ulimwenguni kote, wala hawakupata kuwako, walio na alama sawa ya kidole gumba. Mungu huwafanya watu tofauti, Naye ana karama za namna nyingi na huzituma kwa Kanisa Lake. Lakini tunashikilia tu moja, na hapo mnaenda, mnaona, hampati hekima ya Roho, hiyo ndiyo sababu Mungu hawezi kutuweka mahali ambapo tunapaswa kuwa katika Mwili Wake. Kwa maana mmoja anapewa karama ya namna *hii*, mwingine, karama ya namna *hii*, mwingine, karama ya namna *nyingine*, na kadhalika, bali wote ni Mwili ule ule. Lakini tunataka kufanana kabisa na huyo *mwingine*, huwezi kufanya hivyo, huna budi kutumia hekima ya Neno. Biblia ndiyo iliyo Ramani yetu.

⁹⁶ Sasa, wakati mwana huyu alipowekwa...Mungu alimweka Mwanawe kwa sheria ile ile aliyowakusudia. Sasa, kama Yeye alivyoagiza kwamba kutokutii kutaleta mauti, Mungu alishuka na kufanyika mwili, na akajitwika Mwenyewe uasi, kisha akaifia jamii ya binadamu ambayo Yeye aliweka mauti juu yake, ama, walikuwa wamejiletea mauti juu yao wenyewe, kisha akachukua mauti kwa ajili yao, apate kuwakomboa.

⁹⁷ Katika kuwekwa kwa mwana ambako alikuwa na maagizo ya Agano la Kale, Mungu alishuka na kumweka Mwanawe Mwenyewe mahali pake. Mara walipopanda mlimani, na mara, yule—yule Malaika wa Bwana akaja, ndipo nguvu za Bwana

zikawatia uvuli basi, nayo mavazi Yake yakaanza kung'aa kama jua. Nao wakamwona Musa na Eliya wakimtokea na kuzungumza Naye, ikaja Sauti kutoka Mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye." Alipewa mamlaka yote Mbinguni na duniani, Yeye alikuwa mtiifu. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu basi, Mungu akimweka Mwanawe Mwenyewe mahali pake, sikilizeni: "Msikieni Yeye."

⁹⁸ Sasa, ni kitu gani kilichotukia pale? Mara tu mambo ya kimbinguni yalipofanywa, Petro alisisimkwa sana, kasema, "Nitakwambia tufanye nini, hebu na tujenge vibanda vitatu hapa, tuunde madhehebu matatu mbalimbali, vibanda vitatu mbalimbali. Tutakuwa na kimoja cha wanaotaka kuishika torati ya Musa, tutawaacha waabudu katika maskani hiyo, mtu anayetaka kutimiza msemu wa manabii, tutawaacha waabudie maskani hii, na wale wanaotaka kuamini yale Yesu aliyosema, tutawaweka katika maskani ile."

⁹⁹ Nina furaha sana kwamba Mungu alikomesha hilo. Vipi kama tungaliishika sheria? Sheria ina haki bila huruma. Huwezi kuokolewa kwa sheria, sheria haina wokovu ndani yake. Sheria inakuhukumu tu, inakwambia wewe ni mwenye dhambi na una hatia, bali haina huruma. Ni polisi anayekutupa gereza bila njia yoyote ya kutokea. Nina furaha kwamba haitubidi kumsikiliza Musa, maana alileta torati.

¹⁰⁰ Nao manabii walikuwa ni haki, sitaki haki ya Mungu. La, ninataka rehema Yake, sio haki. Mimi, kama ningalikuwa na haki, ningehukumiwa, nataka rehema. Siombi haki Yake, ninaomba nipate rehema Yake. Musa, ama, Eliya, yule aliyekuwa kwa ajili ya manabii, alipanda mlimani na kuketi kule chini, hakuna mtu aliyepaswa kumkaribia, ndipo mfalme mmoja akatuma watu hamsini. Akasema, "Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, Moto na ushuke na kuwateketeza." Haki, sitaki hiyo.

¹⁰¹ Lakini kabla Petro hajamaliza kuzungumza juu ya vibanda hivyo vitatu mbalimbali, ile Sauti ikanena kutoka Utukufuni na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye. Musa ameondoka, sheria imekwisha, manabii wametoweka, lakini huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye."

¹⁰² Haidhuru mko wapi: "Msikieni Yeye." Haidhuru kitu chochote kinasema nini, kile mama asemacho, kile baba asemacho, kile sheria isemacho, kile chochote kingine kisemacho: "Msikieni Yeye." Yeye ndiye Sauti ya milele. Mungu alimweka mahali pake kama Mpatanishi wako, kama Baba yako, kama Mungu wako. "Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye."

¹⁰³ Marafiki, watu wa taifa hili na ulimwengu huu, ninapouzunguka, ninaona wana njaa sana kwa ajili ya Ukristo halisi, wa kweli. Tuna vya kujibunia vingi sana, kujifanya

kwingi sana, uigaji mwingi sana, mpaka ulimwengu kweli una njaa ya kuona kitu halisi.

¹⁰⁴ Ni pigo la jinsi gani hivi majuzi, wakati Bw. Graham alipoliacha kundi hilo la makafiri kusimama pale na kumpa changamoto kwenye Injili aliyokuwa akihubiri! Sijui ningefanya nini, lakini ninaamini ningekuwa kama wale watoto wa Kiebrania, “Mungu wetu anaweza kutuokoa na kitu hiki.” Kamwe sitaiacha Injili ikanyagwe-kanyagwe.

¹⁰⁵ Angalia, imefikia mahali, rafiki, ambapo ulimwengu ni mbaya sana, utakufanya uthibitishe kila inchi ya ardhi unayosimama, Shetani atafanya hivyo. Na inafikia wakati ambapo uigaji na mawazo ya kimwili yatakatiliwa mbali kutoka kwenye Mwili halisi na wa kweli wa Kristo, Naye atakuwa na Mwili ulio safi, na mtakatifu, na uliojazwa na Roho Wake, ukitembea katika Roho Wake na kufanya kazi alizofanya. Iweni waaminifu kwa hilo.

¹⁰⁶ Wanataka kitu halisi, wanaona njaa na kiu ya kupata kitu kilicho halisi. Hawataki saikolojia, hawataki hotuba fulani ya kiakili, wanataka kitu fulani kinachowapa hakikisho, kitu kinachoifanya Biblia hii iishi tena.

¹⁰⁷ Niliposhuka kwenye ndege huko Bombay, India, ambako tulikuwa na mkutano wetu ulio mkubwa kuliko yote, walikadiria yapata laki tano kuwa kwenye mkutano huo, yule wa kwanza niliyekutana naye kwenye Hoteli ya Taj ambako labda wamishenari mia nne au zaidi walikuwa wamekusanyika pamoja, alikuwa ni askofu wa kanisa la Kimethodisti kule, akaniambia, “Ndugu Branham, huenda nisikubaliane nawe juu ya fundisho lako la uponyaji wa Kiungu.” Akasema, “Lakini una jina zuri, na mimi—mimi nataka ulidumishe hilo safi, kwa kuwa ni kitu fulani kwa watu hawa.” Akasema, “Lakini kamwe usijiite mmishenari hapa,” kasema, “tulikuwa na Biblia hapo awali, miaka elfu mbili kabla hamjakuwa taifa.”

¹⁰⁸ Na hiyo ni kweli, Mtakatifu Tomaso alishuka kule, akaleta Injili India. Lakini walifanya nini? Waliigeuza ikawa theolojia ya kiakili, nayo hapo imewekwa.

¹⁰⁹ Akasema, “Tunasikia, huku India, ya kwamba Mungu amekupa karama ya kuifanya Biblia hii kuishi tena, hilo ndilo tunalovutiwa nalo, kuifanya Biblia iishi tena.” Hilo ndilo watu wenye mioyo yenye njaa wanataka, ni kuona Biblia ikifanywa halisi, kumwona Mungu akijitokeza jukwaani, na kufanya jinsi alivyofanya, Neno lililo hai linakuwa kitu kilicho hai kwetu. Kuona kiu ya mambo yaliyo halisi, uigaji mwingi kupita kiasi.

¹¹⁰ Sijui kama niliwahi kuwasimulia hadithi hii ndogo ama la, ingeweza kuistahimili tena. Kila mtu anajua kwamba mimi huwinda, ninapenda kuwinda, kumezaliwa ndani yangu, siwezi kujizuia. Basi siku moja, nilikuwa nikiwinda huko Northwoods pamoja na jamaa fulani ambaye alikuwa ni mwindaji hodari,

mfuatiliaji mzuri sana, na mlenga shabaha hodari mno. Naye alikuwa ni mtu ambaye haikukubidi kumtafuta wakati wote, a—alijua mahali alipokuwa mwituni. Nami nilifurahia kuwinda pamoja naye.

¹¹¹ Nasi tungeachana, nami ningesema, “Nitakutana nawe maili ishirini mahali fulani, ama *ninii*.” Angekuwa papo hapo. Na kwa hiyo, kamwe hukuwa na wasiwasi kuhusu yeye kugeuzwa au kupotea, mwenyewe alikuwa nusu Mhindi, naye alijua misitu. Kwa hiyo yeye. . .

¹¹² Siku moja nilienda kuwinda pamoja naye. Lakini huyo alikuwa ndiye mtu katili kuliko wote niliyepata kukutana naye maishani mwangu, mwenye moyo katili. Yeye angeninii, alipenda kuwapiga risasi watoto wa kulungu, huyo ni maskini mtoto wa kulungu, ili tu kunifanya nijisikie vibaya, kwa sababu nilikuwa mhubiri, naye angenicheka, na kusema, “Loo, wewe ni mwoga kama kuku. Hiyo ndiyo shida yenu ninyi wahubiri, nyote ni waoga kama kuku.”

Nikasema, “Bert, si hivyo.”

Akasema, “Nilifikiri ulikuwa mwindaji.”

Nikasema, “Mimi ni mwindaji, bali mimi si mwuaji.” Nikasema, “Si—siamini. . . Ninaamini hayo ni mauaji, kufanya tu hivyo kwa ukatili.”

¹¹³ Siamini katika kuua wanyama namna hiyo, kwa kulenga tu shabaha. Kama kuna mtu yeyote ambaye ni mwuaji, ni mzungu. Mpeleke huko Afrika wakati mmoja, mwangalie, ataua mradi tu anaweza kupiga risasi na kuua. Hiyo ni kweli. Iko moja kwa moja ndani yake, asili yake kufanya hivyo. Kuua. . .

¹¹⁴ Maskini Wahindi hawa wanaoketi hapa, jinsi hao walivyowaua nyati wao na kulungu wao, waliokota tu mifupa na kadhalika, wakiwapiga risasi kwa shabaha. Si ajabu wana hisia mbaya juu yake. Mungu aliwapa urithi huo, tukawapiga risasi wote kwa shabaha. Ni aibu, fedheha, doa kwenye bendera ya chochote.

¹¹⁵ Lakini ili kuwa tu mwuaji! Na hivyo ndivyo Bert alivyokuwa, alikuwa tu mwuaji, aliua tu apate kujifurahisha, aliua wanne ama watano katika siku moja, kwa kujifurahisha tu. Mwaka mmoja nilipoenda kule, alikuwa amejitengenezea filimbi ndogo iliyotoa sauti kama mtoto mdogo wa kulungu, jinsi anavyolia, mwajua, akimwita mama yake. Ndipo akanionyesha, nami nikasema, “Bert, hutaitumia hiyo!”

“Loo,” akasema, “jirudie, mhubiri.” Kasema, “Wewe ni mwoga sana kama kuku.”

Nami nikasema, “Bert, ungefanya hivyo?”

“Loo,” akasema, “nifuate tu uone.”

¹¹⁶ Tulienda kuwinda siku hiyo, kama inchi sita za theluji, hali nzuri ya hewa ya kufuatilia, lakini kulungu, baada ya wao kurushiwa risasi mara chache ni wakali sana nchini humo, wale wenye mkia mweupe, wanaweza kujificha wala huwezi kuwaona kuyaokoa maisha yako. Wala hawatatokea mchana, hawatatoka. Kwa hiyo, kama wakiwahi kutoka, utawapata kwenye mapambazuko, ama tu, kabla giza halijaingia, hapo ndipo unapowapata. Nasi tulikuwa tumewinda mpaka yapata saa tano na hata hatukuona mburuzo mmoja, ilikuwa imechelewa kabla hatujaenda kule.

¹¹⁷ Halafu basi, msimu ulikuwa umeendelea majuma kadhaa upande wa kaskazini mwa barabara, ukafunguliwa baada ya Krismasi upande wa kusini wa—wa Safu ya Rais. Kwa hiyo, tulikuwa moja kwa moja nyuma ya Mlima Washington. Basi tulipokuwa tukiwinda siku hiyo, yapata saa tano... Kwa kawaida tulibeba chokoleti ya moto, ina nguvu nyingi kwake, tungeibeba hiyo pamoja na chakula kidogo cha mchana mgongoni mwetu, ambapo kama tungepotea ama kukwama, mbona, tungepata njia yetu, na tuwe na chakula cha kukutia joto kama tungsikia baridi sana; kulikuwa na baridi sana.

¹¹⁸ Ndipo Bert akaketi kwenye kibanda kidogo, chembamba pale, nami nilikuwa nikimfuata, maana baada ya adhuhuri kwa kawaida tulitengana na kuwindia njia zingine tukirudi kupitia kwenye makorongo. Ndipo basi alipoketi pale chini, aliingiza mkono kwenye shati lake namna *hii*, nilifikiri alikuwa akirudi kuchukua chokoleti yake moto. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹¹⁹ ...jike kubwa akainuka, akionekana vizuri sana. Sasa, hilo kwa namna fulani si la kawaida kwao kufanya hivyo, saa tano mchana. Naye akaniangalia kwa mtazamo huo wa aibu. Ndipo huyo jike, akapiga filimbi tena, ndipo huyo jike akajitokeza mahali wazi. Sasa, hilo si la kawaida kabisa. Ungeweza kuona macho yake makubwa mno, ya hudhurungi, na hayo masikio makubwa, yakiangalia kote.

¹²⁰ Bert, kamwe hatukubeba risasi ndani ya bunduki, kwa hiyo akavuta nyuma na kutia risasi, bunduki ilipoalika, yule kulungu akaisikia, naye akaangalia huku na huku, akainuka pamoja na bunduki. Loo, mimi... Hizo nywele za kulenga shabaha katika darubini hiyo zilipitia moja kwa moja moyoni mwake. Nilijua katika sekunde chache, angeulipua moyo wake moja kwa moja kutoka kwake. Ndipo nikawaza, “Anawezaje kuwa katili hivyo?” Nikamnong’onezea, nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

¹²¹ Lakini huyo kulungu hakuwa akijifanya, alikuwa ni mama, alizaliwa mama, kulikuwa na kitu fulani ndani ya mtoto wake mchanga mpendwa. Hivi uliwahi kuona, msichana mdogo anapozaliwa, yeye, anapokuwa mkubwa vya kutosha kutembea, anataka mwanasesere. Ni kitu gani? Kwanza kabisa ni mama, ni

maumbile. Na asili ya huyo kulungu ilikuwa ni kumtafuta mtoto huyo mchanga. Ndipo akageuka na kumwalia maskini yule mwindaji moja kwa moja, akayainua masikio hayo makubwa juu kwa muda kidogo, lakini alijua mtoto huyo mchanga alikuwa taabuni, ndipo akaanza kumtafuta.

¹²² Nilipomwona amelenga shabaha, niliwaza, “Loo, jamani! Unawezaje kufanya hivyo, Bert, kumwua maskini mama huyo aliyesimama hapo namna hiyo, baada ya kumdanganya ati ni mtoto wake anayeita?” Na labda alikuwa na mtoto pale mahali fulani, naye alifikiri alikuwa taabuni, basi alikuwa akimwinda, kwa sababu alikuwa akilia. Sasa, yeye hakuwa akijifanya, huo ulikuwa ni wa kweli, huo ulikuwa ni upendo halisi wa mama.

¹²³ Ndipo alipoanza kupiga risasi namna *hiyo*, niligeuza kichwa changu, nikasema, “Baba wa Mbinguni, unirehemu. Nampenda. Anawezaje kuwa katili hivyo? Huo umama halisi na mwaminifu, naye hapo ataulipulia mbali moyo wake, wakati amemdanganya na kumweka huko nje hadharani. Mama huyo mwenye mtoto hapa mahali fulani, naye anajifanya kama mtoto huyo wa kulungu, akimlilia mama yake!”

¹²⁴ Nami nikangojea kusikia mlilo wa bunduki, nikangojea kwa dakika moja hivi, bunduki haikufyatuka. Nikashangaa, “Kwani kuna nini?” Nikageuka kuangalia, na mtutu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*. Asingeweza kuishikilia tena. Akanitazama huku machozi yakitiririka shavuni mwake, akaitupa bunduki hiyo chini na kunishika kwenye mguu wa suruali, akasema, “Billy, nimetosheka nayo. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake, ambaye ni mtamu sana na amejaa upendo.”

¹²⁵ Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi, aliona kitu cha kweli. Aliona kitu ambacho hakikuwa kikiigiza, hakuwa akijifanya, kweli alikuwa na kile alichokuwa anatenda. Hicho ndicho ulimwengu unachotazamia Kanisani siku hizi, kitu ambacho ni halisi.

¹²⁶ Loo, pamoja na sisi wengine, hivi hungetaka kuwa Mkristo halisi, mwaminifu moyoni mwako kama huyo kulungu alivyokuwa mama? Je, si ungependa kuwa hivyo? Je, ungetaka? Mwaweza kuinua mikono yenu, na kusema, “Ningependa kuwa hivyo?”

¹²⁷ Mungu alisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa; msikieni Yeye. Kazi azifanyazo Yeye, ninyi nanyi mtazifanya.”

¹²⁸ “Kubwa kuliko hizi mtafanya,” ama nyingi, alisema Yesu, “Naenda kwa Baba Yangu.”

¹²⁹ Mungu na awajalie ninyi watu wa Phoenix hapa, ndilo ombi langu, kwamba uaminifu wa Kristo utakuwa moyoni mwenu, uliozaliwa mle ndani kwa asili ya Roho Mtakatifu, ambao utakufanya umwonee Mungu njaa, na kusimama tu mwaminifu kwa Mungu na kwa Neno Lake kadiri ule uaminifu wa umama

ulivyosimama katika maskini—maskini huyo kulungu jike siku hiyo kwa ajili ya mtoto wake.

Na tuombe.

¹³⁰ Je, kunaweza kuwako, kwa bahati, huku mmeinamisha vichwa vyenu...? Ni wenye dhambi wangapi hapa ndani wangetaka kukumbukwa katika maombi tunapofunga usiku wa leo? Mwaweza kuinua mikono yenu? Roshani upande wangu wa kulia, kwanza. Mungu awabariki nyote huko juu, Mungu awabariki. Unataka tu kuwa Mkristo halisi.

¹³¹ Bila shaka siwalaumu, mmeona watu wengi wakijifanya na kuigiza, nayo imewachefua tu, bali unataka kuwa halisi. Ndugu yangu, maskini rafiki yangu uliyepotea, huyo hapo Yesu Kristo halisi, kuna Baba halisi wa Mbinguni, Roho Mtakatifu halisi, Malaika halisi, na kuna Wakristo halisi. Ninaomba ya kwamba Mungu atamfanya kila mmoja wenu hapo kwenye hiyo roshani upande wangu wa kulia, uliyeinua mkono wako, Mkristo kama huyo.

¹³² Hizi roshani zilizo mbele yangu, naomba uinue mkono wako hapo, useme, “Niombee, Ndugu Branham, ninataka kuwa Mkristo, Mkristo tu kama yule kulungu alivyokuwa mama, na uaminifu wangu unaweza kuonyeshwa kwa ajili ya Mwokozi wangu”? Mungu akubariki. Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, hilo ni sawa kabisa.

¹³³ Roshani upande wangu wa kushoto, naomba uinue mkono wako, useme, “Niombee Ndugu Branham, kwamba nitakuwa aina ya Mkristo, kadiri ya Ukristo uliozaliwa ndani yangu, kitu fulani ndani yangu, kwamba ni—nitakuwa mwaminifu kwa Kristo, kama mama yule alivyokuwa kwa wito wa mtoto wake mchanga”? Je, unaweza kuinua mkono wako, mahali popote kwenye roshani upande wa kushoto?

¹³⁴ Chini ya roshani, hapa upande wa kushoto sakafuni, mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu akubariki, bwana, Mungu awabariki nyote huko chini, hilo ni sawa kabisa. Nyote huko nyuma, Mungu awabariki, hilo ni zuri.

¹³⁵ Kwenye marefu ya katikati yaliyonyoka hapa, ni wangapi mngeinua mikono yenu, na kusema, “Nikumbuke”? Mungu awabariki, moja kwa moja huko nyuma kabisa. Ninaona hata huko nyuma kabisa kwa watu weusi pale, ninawaona. Mungu awabariki. Atawafanya hivyo.

¹³⁶ Sasa, chini ya roshani upande wa kulia, na marefu haya hapa ndani, ni wangapi ungeinua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham.” Mungu akubariki, hilo ni zuri, hilo ni sawa. Mungu na awarehemu.

¹³⁷ Sasa, kwa ninii yangu, hapa nyuma yangu, hapa nyuma. Mungu awabariki. Hilo ni sawa. Nimekuwa nikiwakosa hapa

kwa siku kadhaa usiku. Lakini Mungu akiwa pamoja nanyi sasa, na awajalie, awape shauku ya moyo wenu.

¹³⁸ Sasa, ninataka kila mmoja wenu uliyeinua mkono wako muombe pamoja nami, nami ninawatakeni mumwamini Mungu kwa moyo wenu wote. Sasa, kuna Kitu fulani kilichokufanya uinue mkono wako, ilikuwa ni Kitu fulani unachotaka kuona ambacho ni halisi. Ninawatakeni mume Mungu ahadi usiku wa leo, kama mtamwona Yeye akiingia kwenye mstari huu wa uponyaji na kufanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani: alijua siri za moyo, akawaponya wagonjwa na wanaoteseka, akawafanya viwete kutembea, vipofu kuona, viziwi kusikia, bubu kunena, hatujui ni kitu gani kitakachokuwa hapa ndani, kama akifanya hivyo, basi mtaona onyesho la Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu halisi, basi ninawatakeni mje, mara tu i—ibada ya uponyaji itakapokwisha, huku juu, na kusimama kuzunguka madhabahu hapa ambapo mnaweza kuombewa. Ndipo basi mhudumu fulani anaweza kukuchukua kama mchungaji kwa—kwa kundi lake, na huko awalishe na kuwatunza, mpaka mtakapowekwa katika ule Mwili.

¹³⁹ Baba yetu wa Mbinguni, kulikuwako na baadhi, labda mikono thelathini hadi hamsini usiku wa leo, kila mahali, wote kwenye roshani, na wote chini ya roshani, huko nje katikati ya sakafu, watu wengi waliinua mikono yao, vijana, na wazee, na watu wa makamu, wote wakitaka kuwa halisi, wanataka kuwa Wakristo halisi. Wanataka kuwa na, si kabadala, kitu ambacho iliwabidi kumwiga mtu fulani, bali tukio halisi walilopewa na Mungu pekee, ambalo linawafanya Mkristo halisi, mwaminifu. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utamjalia kila mmoja baraka hii.

¹⁴⁰ Wabariki wale, Bwana, ambao wamerudi nyuma usiku wa leo, ambao hawatembe katika imani tena, ambao wameenda kando kutembea katika ulimwengu huu wa sasa, wakiupenda kuliko wanavyompenda Kristo. Ninaomba ya kwamba utawageuza usiku wa leo, na jalia waone kitu fulani halisi sana usiku wa leo, hata wataninii, kitavutia usikivu wao kama vile kijiti kilichowaka moto kilivyomvutia Musa, na jalia waingie katika ushirika mtamu tena pamoja Nawe na pamoja na Kanisa. Tujalie, Baba.

¹⁴¹ Pia libariki Kanisa lote. Na jalia wakae wamekaribiana, katika upendo na ushirika, makanisa yote na makundi yote ya waaminio, mpaka tutakapomwona Mwana mkamilifu wa Mungu akiumbika miongoni mwetu, kuurudisha mwili halisi wa Kristo. Ndipo miili ya hao waliolala katika Yeye itabadilishwa na kufanywa kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo Yeye anaweza kuvitiisha vitu vyote chini Yake. Tujalie, Baba.

¹⁴² Ninaomba jambo hili sasa, ya kwamba Wewe utajitokeza jukwaani kama tulivyohubiri asubuhi ya leo, Mungu wa historia

ajitokeze jukwaani, Mungu yeye yule, kuwafanya watu wajue ya kwamba, “Msiogope, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” Jalia Sauti ya Mungu ivume mioyoni mwao usiku wa leo: “Huyu ni Mwanangu, mpendwa; msikieni Yeye.” Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

¹⁴³ Tumeketi hapa usiku wa leo, chini ya matarajio makubwa sasa, tuingojea, mstari wa maombi. Ninaamini Billy aliniambia aligawa kadi hamsini za maombi usiku wa leo. Hiyo ilikuwa ni kweli? C? A, B, C? Mara ya tatu tuliyogawa kadi za maombi. Wao si. . . Niliwauliza jinsi mlivyotaka mkutano ufanyike, na nyinyi mliomba kadi za maombi usiku wa leo, kusudi kundi lote liweze kuja huku na kuwekewa mikono. Hilo ni zuri sana, Maandiko yanasema hivyo.

¹⁴⁴ Sasa, kusudi wasije wakachanganyikiwa. . . Hiyo ndiyo sababu hatuwezi kumleta kila mtu, si uwanja wa michezo, mwajua, ni uwanja wa michezo, bali sasa ni kanisa. Ndugu watapigana na ndugu kesho usiku, lakini sisi tunapigana na ibilisi usiku wa leo, katika uwanja huu. Lakini tunataka kuufanya kanisa la Mungu.

¹⁴⁵ Ni nani aliye na kadi ya maombi C? C kama katika Christ [Swahili: Kristo—Mfa.]. C, namba 1, waweza kuinua mkono wako? Mtu aliye na C, namba 1. Kadi ya maombi. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁶ . . . upindo wa vazi la Yesu, ndipo akauhisi ugonjwa wake. Wakati alipomgusa, yeye, Yeye alihisi imani yake na kuuangalia umati, kisha akamwona, na kumwambia ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Ni wangapi wanaojua hayo kuwa ni Maandiko? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu hakudai kuwa mponyaji, ya kwamba Yeye alisema, “Mimi. . . Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana”? Yohana Mtakatifu 5:19. Duniani, alipokuwapo.

¹⁴⁷ Vema, hivi. . . ? Ni wangapi hapa wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo hajafa, kwamba Yeye yu hai? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Biblia ilisema katika—katika Waebrania 13:8 ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Vema, kama Yeye ni yule yule, Yeye ni yeye yule katika kanuni, yeye yule katika nguvu. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye alisema kwamba kitambo kidogo na hakuna mtu angemwona tena, maana alikuwa anaenda kupaa Juu?

¹⁴⁸ Lakini haya ndiyo yangetukia: Yeye angekuwa Mzabibu nalo Kanisa lingekuwa ni matawi. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba, mzabibu sio unaozaa matunda, ni tawi? Tunda hutoka kwenye tawi. Basi kama “ninyi ni matawi,” hilo ni Kanisa, washiriki wa hilo Kanisa, ule Mwili. Vema. Basi kama tawi, lile, liko ndani ya Mzabibu, hilo tawi

litazaa matunda ya huo Mzabibu. Hiyo ni kweli? Basi hayo ni Maisha ya Kristo Kanisani yakizaa matunda yale yale aliyozaa Yeye.

¹⁴⁹ Aliwafanyaje watu wajue Yeye alikuwa ni Masihi? Sasa, je, Mataifa walikuwa wakimtazamia Masihi katika siku hiyo? La, bwana, walikuwa makafiri. Vema. Je, Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi? Naam. Je, Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi? Naam. Alijitambulishaje kwa hao wawili? Kuna watu watatu tu, kwa vyovyote vile: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, kulingana na Biblia, wana wa Nuhu. Hao ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Mnaamini hilo?

¹⁵⁰ Ni wangapi wanaojua ya kwamba Petro alipewa funguo za Ufalme? Aliwafungulia lini Wayahudi? Pentekoste. Hiyo ni kweli?

¹⁵¹ Aliwafungulia lini Wasamaria? Wakati Filipo aliposhuka kwenda kule na kuwahubiri, na kuwabatiza, walikuwa na uamsho mkubwa, Roho Mtakatifu alikuwa amewashukia, Petro alikuwa na funguo, wakashuka, wakawawekea mikono yao, wakampokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli?

¹⁵² Mataifa waliupata lini? Nyumbani mwa Kornelio, yule Mrumi. “Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia wale waliolisikia Neno.” Hiyo ni kweli?

¹⁵³ Lakini wakati Yesu alipokuwa hapa, Yeye alijidhihirisha tu kwa Myahudi na Msamaria, ndio wawili tu waliokuwa wakimtafuta. Alipofanya hivyo, aliwafanyaje wajue ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi? Musa alisema, “Masihi ajapo, Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Itakuwa, yeyote asiyemsikia huyo Nabii atakatiliwa mbali na watu.”

¹⁵⁴ Sasa, Masihi huyu hana budi kuwa ni Mwanadamu (Hiyo ni kweli?), aliyezaliwa na bikira, na angefanya ishara ya nabii, Nabii mkuu. Hiyo ni kweli? Petro alipoambiwa yeye alikuwa ni nani, kasema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.” Alimwabudu na kujua ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi.

¹⁵⁵ Wakati Filipo alipoenda akamwona Nathanaeli chini ya mti, na kumrudisha mbele za Yesu, Yesu alimtazama, akasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!” (Niambi ni mtakapokuwa tayari...?) “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

¹⁵⁶ Ndipo aliposema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁵⁷ Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ni macho ya jinsi gani!

¹⁵⁸ Naye akasema nini? “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu.” Alimtambuaje? Kwa ishara. “Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Ndivyo alivyo.

¹⁵⁹ Ndipo aliposhuka kwenda kwa Wasamaria, alikuwa na haja ya kupitia huko. Wanafunzi wakaingia kununua chakula, Yeye akaketi kwenye, kwenye uzio mdogo wa vipandio karibu na kisima, kisima cha umma pale. Mwanamke, kahaba, tunavyomjua, akatokea, akaanza kuteka maji, ndipo Yesu akamwambia, na kusema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹⁶⁰ Akasema, “Si kawaida, tuna ubaguzi. Ninyi Wayahudi na sisi hatuna uhusiano sisi kwa sisi. Si haki Kwako, ukiwa ni mwanamume wa Kiyahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho.”

¹⁶¹ Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Basi mazungumzo yakaendelea mpaka Yesu akapata mahali shida yake ilipokuwa. Kuna mtu anayejua shida yake ilikuwa ni nini? Alikuwa anaishi katika uzinzi. Ndipo Yesu akamwambia, akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Umeishi na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Umesema kweli.”

¹⁶² Yeye alisema nini? Alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.” Sasa sikilizeni, si hayo tu. “Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake.” Ni wangapi wanajua Maandiko yanasema hivyo? “Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuonyesha mambo yote. Lakini u nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁶³ Ujumbe wake ulikuwa nini sasa? Akakimbilia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

¹⁶⁴ Sasa, Mungu hana kikomo, mnaamini hilo? Hawezi kubadilika, hakuruhusu hata mmoja wa watu hao, makabila ya watu, kusitisha kizazi chao bila kuiona ishara hiyo. Yeye alitabiri ya kwamba Mataifa wangeipokea kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma. Sasa, kama Yeye aliwapa ishara hiyo, na kutuacha tu tuingie kwenye mambo ya kiakili, Yeye alituhadaa kwa kitu fulani. Hatafanya hivyo, ni yeye yule. Kama hilo lilikuwa ni wazo Lake, kama hilo lilikuwa ni ninii Yake. . .

¹⁶⁵ Mungu kamwe anapoitwa jukwaani, jinsi Mungu anavyotenda mara ya kwanza, hana budi kutenda, milele, hivyo, kama sivyo, Yeye alikosea mara ya kwanza, alifanya kosa. Lakini mnaona, Mungu anapotenda, Yeye hutenda vile vile kila wakati.

¹⁶⁶ Kama mwenye dhambi aliitwa, Naye akamwokoa huyo mwenye dhambi, mwenye dhambi anayeitwa tena, hana budi kumwokoa, mwenye dhambi mwingine, mwenye dhambi mwingine, mwenye dhambi mwingine, mwenye dhambi

mwingine, na wote wanaoita. Kama mtu akiomba apate uponyaji wa mwili wake, na Mungu amponye, basi mwingine, mwingine, mwingine anayeita hana budi kuponywa, juu ya msingi wa imani kwa yeyote.

¹⁶⁷ Aliwaonyesha Wayahudi ile ishara ya Masihi kabla ya kipindi chao cha wakati kumalizika, aliwaonyesha Wasamaria ishara ya Masihi kabla ya kipindi chao cha wakati kumalizika, lakini hata wakati mmoja hakuonyesha Mataifa hilo, hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote, sasa wanamtazamia. Huyu hapa Masihi yeye yule aliyetabiri ya kwamba angefanya hivyo, akirudi moja kwa moja miongoni mwa watu, si mimi, *sisi*, Kanisa, ulimwenguni kote, tukirudi, tukionyesha mambo yale yale aliyofanya papo hapo. Hatuna budi kuliamini.

¹⁶⁸ Sasa, ninyi mnaotaka kuona kitu ambacho ni halisi, kitu ambacho ni cha kweli, hebu Roho Mtakatifu na aweze kuwapa hicho usiku wa leo.

¹⁶⁹ Mlisema ni wangapi waliokuwa hapa bila kadi za maombi? Inua mkono wako. Bila shaka huninii, ninamaanisha wagonjwa, kadi za maombi mstarini. Sasa ombeni kwa dakika moja tu, wakati wakimalizia mstari huo. Hebu kidogo.

¹⁷⁰ Wasemaje? [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, sawa. Ninii tu, ni sawa. Hebu kidogo, ninajaribu kuwashughulikia watu huko nje sasa wasio na kadi.

¹⁷¹ Ninaendelea kuwazia juu ya saa hiyo, bali sijui ni lini tutawahi kukutana tena. Hebu tutulie kwa dakika moja, tunyamaze. Mkianza kusukumana, ndipo ibilisi anaanza kulishughulikia hilo, mnaona, akijaribu kulifanya kitu ambacho sicho.

¹⁷² Sasa hebu na tuwe na imani na kuamini. Hebu tuamini tu kwa mioyo yetu yote ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa, tayari kutupa kile tunachotaka. (Paul, wote wako tayari?) Ninataka kote humu jengoni, kila mahali mlipo, ninawatakeni mwombe.

¹⁷³ Sasa nataka kuwaulizeni swali kabla sijafanya hivyo. Angalieni hapa, mpate kujua unyofu. Biblia hii, ninayopenda na kuamini kuwa ni Neno la Mungu, Malaika huyo mnayemwona kwenye picha. . . Vema, si lazima niwaambie, Yule pale kwenye picha. Yule pale Bw. George J. Lacy, wa FBI, alama za vidole na hati, anathibitisha ya kwamba ile Nuru ilikuwa pale na ikagusa lenzi, si saikolojia. Akasema, “Jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia.” La, la hashia.

¹⁷⁴ Kwa hiyo, Mungu akiwa ndiye hakimu wangu, ninaiona Nuru hiyo. Kwa ufunuo, kwa ono. . . Kama sitakutana nanyi tena, mpaka nitakapokutana nanyi katika Nchi ya Utukufu, na kusimama Siku hiyo kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo ambapo sote tutakuja, nimewaambia ukweli. Najua mnafikiri kwamba kutoelimika kwangu. . . Mimi si mhubiri sana, maana

sina elimu, lakini Mungu alinipa tu karama, hiyo ni kumwondoa tu William Branham njiani, kusudi Yeye aweze kuchukua hilo ganda na kunena kupitia kwake Mwenyewe.

¹⁷⁵ Sasa ninyi ombeni, nami nawatakeni mwe waaminifu. Na kama Mungu atafanya na kutenda papa hapa usiku wa leo, kama tu alivyofanya wakati alipokuwa katika mwili hapa duniani, akitenda kupitia miili yetu, kufanya ishara zile zile, maajabu yale yale, basi ninawatakeni mfanye hivi: ushikilie msalaba mpaka Mungu atakapokuweka, kimahali, mahali anapokutaka katika Mwili wa Kristo. Mungu, tujalie.

¹⁷⁶ Iko nyuma yangu. Mama huyo ameketi mwishoni mwa safu hiyo hapo, u—unamtaka Mungu, sivyo? Kama Mungu atanielezea shida yako, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utaamini? Ulikuwa na ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Sasa, sikujui. Je, una kadi ya maombi? La, wewe, bila shaka huna. Vema.

¹⁷⁷ Sasa, unaamini ninii yangu...? Unaamini hiyo ni kweli? Unaamini huyo angekuwa ni Roho yeye yule aliyemwambia yule mwanamke alikuwa na waume watano? Unaamini kwa moyo wako wote, basi huna budi kuponywa. Unaona? Sikujui, sijawahi kukuona. Uligusa kitu Fulani, Naye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Kama Kuhani Mkuu angeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, si angetenda kama alivyotenda wakati huo kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule?

¹⁷⁸ Hilo lilimfurahisha mwanamke huyo aliyeketi karibu nawe. Wewe ndiwe uliyemvuta Roho wa Bwana. Unaamini, mama, kwamba Mungu anajua shida yako? Kama nitakwambia kutoka hapa shida yako, utakubali uponyaji wako? Ingekusaidia? Kivimbe kwenye sikio lako, unakiombea. Hiyo ni kweli, sivyo? Una imani? Amini sasa.

¹⁷⁹ Vipi kuhusu huko kwenye kusanyiko hapa? Huyu mtu aliyeketi hapo, kichwa mkononi mwake akiomba, ambaye ana ugonjwa wa tezi na wasiwasi, kama utaamini, bwana, utakuacha, nawe unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Unakubali uponyaji wako? Unaamini kwa moyo wako wote? Vema. Ulikuwa ukiomba wakati huo, hiyo ni kweli. Yesu anakuponya.

¹⁸⁰ Mwanamke huyo moja kwa moja nyuma yake hapo, unaamini Mungu angeweza kuniambia shida ni nini? Unaamini miguu yako ingepona? Unaamini? Imekuwa ikikusumbua kwa muda. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bi. Hershey? Hiyo ni kweli. Vema, unaweza kwenda nyumbani sasa na uwe mzima kama unaamini. Inua mkono wako, useme, “Ninamsifu kwa ajili ya jambo hilo.” Vema.

¹⁸¹ Mwaminini Mungu, aminini. Vipi kuhusu mtu fulani kupitia hapa, baadhi yenu watu, kwa hiyo ninyi. . .

182 Yupo mtu aliyeketi papa hapa akiomba. Simjui, sijawahi kumwona. Ana yabisi kavu. Huyu ni mke wake ameketi karibu naye, ana yabisi kavu, pia. Amini unaukosa. Bw. Rinehart, amini kwa moyo wako wote, simama ukaponywe, wewe na Bibi Rinehart, Yesu Kristo anakufanya mzima. Amina. Amini sasa. Amina.

183 Hmm! Utukufu! Ee Mungu, kwa nini watu hawawezi kuiona Hiyo? Msifikiri mimi nina kichaa, sina. Kwa nini . . . ? Inaonekana kwangu kana kwamba hilo lingetia moto mahali fulani! Hivi hamwezi kuiona hiyo? Ni Mungu aliye hai akijifanya Mwenyewe halisi.

184 Maskini mwanamke huyo wa Kihindi aliyeketi huko nyuma, shinikizo la damu, amini, dada, uponywe. Unaamini? Amevaa nguo ya waridi, akiniangalia. Vema. Unaamini hilo shinikizo kuu la damu limeondoka? Vema. Punga mkono wako kama unaamini umekwisha. Vema. Mungu akubariki. Mungu anakupenda.

185 Hilo lilimchangamsha sana msichana mwingine wa Kihindi aliyeketi kule nyuma, kumwona yule mwanamke mwingine. Unaamini Mungu anakuondolea huo ugonjwa wa mgongo, dada, uliyevaa maskini ninii nyeupe. . . huko nyuma? Unaamini Yeye angechukua . . . kuufanya mgongo wako mzima?

186 Huyu Mhindi aliyeketi karibu naye ana ugonjwa wa mapafu, aliye karibu naye ana ugonjwa wa mgongo, pia. Huwezi . . . Mnaona, Mungu anajua yote kuwahusu. Mnaamini Mungu atawaponya, kila mmoja wenu, mlioketi huko nyuma kwenye safu ya nyuma? Je, mnaweza kuelewa Kiingereza? Vema. Amini tu kwa moyo wako wote basi, uponywe.

187 Yuko wapi mwanamke yule ambaye mtu fulani alimtambulisha hapa? Ni huyu mama aliyesimama hapa? Angalia hapa, mama. Unaniamini mimi ku . . . ? Mwanamke huyo yuko mstarini? Loo, kwa nini yeye hayuko huku juu . . . ? Hawezi kusimama, sawa. Angalieni hapa, kama Mungu atafunua shida ya mwanamke yule aliyesimama pale, je, ninyi wengine mstarini mtaamini ili tuweze kuwaombea watu wote? Unamwamini kwa moyo wako wote sasa? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba hilo ni halisi? Ni wangapi wanaoamini hilo ni halisi liwezavyo kuwa? Nawatakia heri, hilo ni zuri. Sasa, wewe weka Roho huyo moja kwa moja juu yako namna hiyo, dumisha upako huo. Wewe pia, bwana.

188 Vema, kwa kweli sana sana hujiombe mwenyewe. Kuna swali moyoni mwako ambalo unaombea, ambalo ni kubwa kuliko kwa ajili yako mwenyewe. Hiyo ni kweli, sivyo? Ni kweli. Sikujui, nijuavyo mimi, sijawahi kukuona maishani mwangu, bali Mungu anakujua. Kama Mungu atanifunulia kilindi hicho ni cha nini, inaonekana kana kwamba roho yako inaendelea kurudi nyuma, kama Mungu anaweza kunifunulia hicho ni kitu

gani, ungekubali, kama ukikipata, chochote ulichoomba? Je, watu wengine wangeungana naye?

¹⁸⁹ Ni kwa ajili ya mtu mwingine anayemtetea, huyo ni mwanamke, mwenye umri mdogo sana kuliko alivyo yeye. Loo, ni binti yake. Binti ametiwa uvuli wa mauti, ana kansa. Hiyo kansa, amefanyiwa upasuaji kwa ajili yake, na hiyo kansa, ha—haikufanikiwa, wasingeweza kuikomesha. Hiyo kansa iko kwenye mishipa ya damu, kuna mbili.

¹⁹⁰ Nawe kwa namna fulani ni mlemavu, wewe, sababu usingeweza kupanda vipandio, unatembea kwa kijiti, ama fimbo, ama, kuna kitu fulani unachotembelea, ninakuona ukijaribu kuondoka barabarani. Hiyo ni kweli. Umekuwa katika mikutano yangu hapo awali. Uliombewa wakati mmoja katika mkutano wangu, na ulikuwa na tatizo fulani ambalo, ilikuwa, wewe, vigumu kupumua, pumu, ndipo Bwana akakuponya hiyo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini kwa moyo wako wote? Loo, kweli unaamini?

¹⁹¹ Sasa, unajua sikujui. Sijui nilichosema, kiko kwenye ile kanda pale chini. Mungu anajua, huku mkono wangu ukiwa juu ya Biblia yangu, kadiri nijuavyo sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Schaeffer, unaweza kwenda nyumbani sasa, Yesu Kristo atakupaja haja yako.

¹⁹² Sema, “Bwana asifiwe.” Hivi huamini?

¹⁹³ Sasa unatambua mama, ningejua shida yako. Lakini lolote ningesema ama chochote kile, hilo lisinge—lisingekufaa kuliko vile tu ungeweza ku—kuombewa tu, hilo lingefanya, sivyo? Lakini unafikiri utakuwa mlemavu? Unafikiri Mungu atakuponya, na yabisi kavu, na kadhalika, itakuacha, utakuwa mzima? Unaamini? Hayo tu ndiyo unayopaswa kujua. Amini tu kwa moyo wako wote.

¹⁹⁴ Waweza kuja? Sasa, unajua ninajua shida yako, sijui, Mungu anajua, lakini ningeweza kukwaambia. Unaamini ya kwamba Mungu angeweza kunifunulia? Ingekusaidia? Je, wewe ni Mhispania? Wewe ni Mhispania. Je, hilo lingewasaidia Wahispania, mnafikiri, kama ningewaambia shida yako ilikuwa ni nini? Unafikiri ingewasaidia?

¹⁹⁵ Watu wa Kihispania wanaoamini, ingewafanya muamini? Huyu ni dada yenu, dada yangu, pia. Sivyo? Vema basi, kisukari kitakuacha, unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Unaamini hilo? Vema, basi unaweza kwenda zako na kufurahi.

¹⁹⁶ U hali gani? Vema, unaamini ya kwamba watu wote weupe huko nje wameamini kama Mungu angeniambia shida yako ni nini? Basi wasiwasi wako utakuacha, karibu wote huko nje wanaugua huo, kwa vyovyote vile. Mnaona? Nao utakuacha, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Mungu akubariki sasa.

- 197 Kuwa na imani, amini. Unaamini kwa moyo wako wote?
- 198 Loo jamani, maskini ugonjwa huo wa pumu, unaamini Mungu atauponya? Vema, katika Jina la Bwana Yesu, nenda ukaponywe.
- 199 Sasa, kwa Wahindi, huyu hapa dada yenu, Wahindi. Ni Wahindi wangapi walio hapa ndani wanaoweza kuelewa Kiingereza? Inua mkono wako, Wahindi. Vema, huyu hapa dada yenu, dada yangu, pia. Sijawahi kukutana naye maishani mwangu, sijui lolote kumhusu. Kama Mungu ataniambia shida yake, mnaamini ni Roho yeye yule aliyemwambia yule mwanamke shida yake ilikuwa ni nini? Mtaamini, enyi Wahindi?
- 200 Unaelewa Kiingereza vizuri? Moyo wako utakuwa mzima, nenda. Amina. Amini.
- 201 Tatizo lako liko mgongoni mwako. Nenda, amini na uponywe. Amini, usitie shaka.
- 202 Kwanza kabisa una yabisi kavu, ugonjwa wa tezi na yabisi kavu. Amini kwa moyo wako wote, nenda, uponywe.
- 203 Ugonjwa wa wasiwasi, nenda, uponywe, amini.
- 204 Unaamini kwa moyo wako wote? Vema, hebu na tuseme, "Bwana asifiwe."
- 205 Unasumbuka sana kuhusu jambo fulani. Unahofu jambo fulani limetukia, sivyo? Unaamini Bwana Yesu anaweza kukuponya, ugonjwa wa rektamu? Unamwombea mtu mwingine. Nimemwona akisimama mbele yangu wakati uo huo tu. Ni ndugu yako. Ndugu yako hayuko hapa, yuko California. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Pumu. Endelea tu uamini sasa. Unaona? Nenda ukiamini. Naam, usi—usininii. . . Unaona?
- 206 Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? Wako? Vema, basi nenda ukaamini.
- 207 Hebu tuseme, "Bwana asifiwe." Kila- . . .
- 208 Sasa, ni wangapi wenu mtaungana nami kwa mioyo yenu yote sasa, na kuomba sasa tunapowaombea watu hawa? Linanifanya dhaifu sana, unakuwa kama, wewe ni kivuli tu ukicheza-cheza mbele yangu. Hebu na tuombe kidogo tu, ninyi ombeni pamoja nami sasa.
- Njoo, dada.
- Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu, ninamwombea dada yetu, ya kwamba utamponya.
- "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."
- Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe, Bwana, katika Jina la Yesu.
- Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe.

Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya dada. Mungu, ameponywa mara nyingi sana, ninaomba ya kwamba utamjalia tena, kupitia Jina la Yesu.

[Dada huyo anasema, “Mungu akubariki, ndugu.”—Mh.] Sawa.

Baba wa Mbinguni, ninamwomba dada yetu, ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo.

Mungu, ninamwomba mvulana huyu mdogo, ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁰⁹ Mungu, ninamwomba dada aliye na kanisa hili kuu usiku wa leo, tukiweka mikono juu yake kama waaminio, katika Jina la Yesu. Weka mikono juu yake, na umtake ibilisi aondoke, katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaelewa ninalomaanisha?

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe.

Njoo dada, unamwamini sasa?

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe. Amina.

²¹⁰ Vema. Una wasiwasi? Unahofia upasuaji huo wa uvimbe huo, lakini utakuacha kama utaamini. Unaamini? Basi nenda ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.” Unaona?

²¹¹ Mnaamini, ninyi nyote? Mnaona? Ninafanya hivyo tu kwa ajili ya kupumzika kidogo kwa dakika moja tu. Unaninii tu. . . Mungu anajua kila moyo, lakini Yesu, wakati mwanamke mmoja alipomgusa, Yeye alisema nguvu zilimtoka. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua hizo ni uweza? Hakika, ndivyo ilivyo.

²¹² Ingekusaidia kama ningekwambia shida yako ilikuwa ni nini? Ingekusaidia? Vema. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mama yako, ni mahututi sana. Ana kansa na ugonjwa wa moyo, dhaifu sana hana budi kudungwa sindano. Hiyo ni kweli, sivyo? Unampenda, Mungu anampenda. Naomba umpate katika hali ambayo—ambayo unataka awe, ndilo ombi langu.

Mungu wa Mbinguni, mponye katika, Jina la Yesu.

²¹³ Nenda, gusa lesa hiyo, unaona, kwa ajili yake. Nenda, ukiamini sasa.

Njoo, dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Tujalie, Bwana.

Njoo, dada mpendwa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Ee Mungu wa Milele, ninambariki mwanamke huyu na mtoto. Jalia nguvu za Mungu zije juu yao na kuwasaidia. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

Mungu akubariki, dada, amini sasa.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba umbariki ndugu yangu, Baba, wakati kanisa hili kuu linapomwombea.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, Mungu, naomba umbariki dada yangu na kumponya. Amina.

Njoo, dada. Unaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, ninagusa mkono wa mwanamke huyu, ninaomba kwamba aponywe.

Njoo dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba, Mungu, ya kwamba utamgusa na kumponya, katika . . .

²¹⁴ Sasa, usiwe na wasiwasi kuhusu mikono hiyo, dada. Usi—usi—usiwe na wasiwasi, endelea tu kuamini, itakuwa sawa.

²¹⁵ Unaamini Mungu atakuponya? Tezi ni mbaya, zina kansa. Lakini unaamini Mungu atawafanya waponywe na kuwapa afya?

²¹⁶ Basi, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya, na ili kwamba aweze, aweze kuwa mzima tena. Ninamkemea ibilisi huyu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²¹⁷ Vema. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, atakuponya tumbo, akufanye utembe na uwe mzima tena?

Mungu, ninaomba ya kwamba utatujalia. Katika Jina la Yesu. Amina.

Njoo, ndugu.

Mungu Baba yetu, ninaomba katika Jina la Yesu, ya kwamba utamponya.

Njoo, maskini mama. Unaamini Bwana Yesu atakuponya? Sawa.

Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya huyu msichana mpendwa, maskini, msichana wa Kihindi na kumpa afya, katika Jina la Yesu. Amina.

Unataka kuponywa? Basi utakuwa sawa, dada.

Baba wa Mbinguni, ninamwombea dada yetu, na kuomba ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu. Amina.

²¹⁸ Mungu ambariki mvulana huyu mdogo. Ninaomba, Baba Mungu, ya kwamba utamponya na kumpa afya, na ili aweze kwenda na kucheza na kuwa kama wavulana wengine, katika Jina la Yesu.

Unajua Yesu anaweza kukuponya? . . . ? . . . Hiyo ni kweli.

Baba wa Mbinguni, ninamwombea ndugu yangu na kuomba ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu. Amina.

Njoo, ndugu mpendwa.

Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utaondoa udhaifu na ulemavu kutoka kwa ndugu yangu, na kumponya. Katika Jina la Yesu. Amina.

Unaamini, maskini mama?

Katika Jina la Yesu Kristo, Roho Mtakatifu na amponye na kumpa afya. Amina.

Unaamini sasa, dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe na uwe mzima. Amina.

Unaamini, dada mpendwa?

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yangu na aponywe. Amina.

Bwana Mungu... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

219 Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kukupa afya? Una sikio lenye shida, huwezi kusikia vyema kutoka kwake. Ulipata ajali, muda mrefu uliopita, ukaumiza kichwa chako, kifua chako. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, kukufanya usikie masikioni mwako tena, vizuri? Vema, unaamini. Na tuombe.

220 Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja.

221 Katika Jina la Yesu Kristo, ninamkemea ibilisi huyu. Toka kwa mtu huyu!

222 Umekuwa hivi kwa muda gani? Ati muda gani? 1944? Unaona unasikia kutoka kwa masikio yote mawili? Unanisikia? Unanisikia?

223 Sasa unaweza kuinua kichwa chako.

224 Angalia hapa. Unanisikia? Unanisikia? Umeponywa. Ninaona una kitu ambacho umekuwa ukijaribu kushinda kwa muda mrefu, tabia. Nenda, uziache usiku wa leo, amini, sigara hazitakusumbua tena. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Nampenda, nampenda

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

225 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa kwa muda kidogo tu, tafadhalini, nashangaa sasa: Kuna wale hapa ambao wangetaka kuja karibu na madhabahu, na kusema, “Ninaamini, Mungu, ya kwamba nimemwona Roho Mtakatifu halisi akitenda kazi miongoni mwa watu”? Je, ungependa kufanya hivyo? Tunapoinamisha vichwa vyetu na kuimba tena, kila mtu tafadhali, kama utainamisha kichwa chako, na hebu tuombe na kuimba. (Ndugu Borders, ongoza huu. Ninapwelewa na sauti.)

226 Njoni huku karibu na madhabahu hapa, na msimame hapa kwa ajili ya maombi. Mtafanya hivyo? Wewe uliyeinua mkono

wako unayetaka kumwona Mungu anayejua siri za moyo wako. Hiyo ndiyo njia, mama, hiyo ndiyo njia. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapoimba.

Nampenda, nampenda . . . 

60-0313 Msikieni Yeye
Madison Square Garden
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org